NAMNA YA KUTUMIA KITABU HIKI:

(Maagizo kwa kiongozi wa kikundi)

1. Kwa sababu ya sili ya masomo haya na hitaji la kubadili fundisho kwa mahitaji ya wanafunzi, ni bora ikiwa kiongozi akiwa na nafasi ya kusoma kupitia fundisho kila juma kwa nafasi yake.

2. Ikiwa itawezeka, na washirika ni wenye kujua kusoma na kuandika, itakuwa vizuri ikiwa kila mmoja atahimizwa kuleta daftari kila juma katika mafundisho.

3. Kwenye mwanzo wa kila somo, omba kwamba MUNGU atafanya kazi katika maisha ya kila mshirika akimfunulia kweli zake.

4. Siku zote fanya marudio kabla ya kuanza hadithi mpya, lakini jisikie huru kuongeza maswali, kubadili maswali, au kupunguza maswali kufuatana na uwezo wa kila kundi.
5. Soma hadithi ya Biblia, lakini uwe mwangalifu usije ukasimama katikati ili kufundisha – sehemu ya kufundisha itafuata baadaye.

6. Uliza maswali ya mdomo mwishoni mwa hadithi.

7. Ikiwa utahisi kuwa kundi linautata katika kuelewa baadhi ya sehemu za hadithi, rudia kusoma tena hadithi ili kwamba itaeleweka vema kwa wote. Hii ni muhimu kabisa ikiwa kundi halina desturi za Ukristo tangu huko nyuma.

8. Kutegemeana na washiriki, baadhi ya mafundisho yanaweza kuchukua muda mrefu zaidi kuliko saa moja iliyopangwa hadi saa moja na nusu. Ikiwa itakuwa hivyo, kiongozi anaweza akatenga hadithi na kufanya nusu kwa juma moja na nusu ingine kwa juma lingine. Kwa mfano fundisho la pili linaweza kutengwa “KUKIMBIA KWA YESU” juma moja na “KUBATIZWA KWA YESU” juma linalofuata. Ikiwa hii haiwezekani, kiongozi anaweza kutaka kufundisha kila kweli moja ya kweli za kiroho pekee kwa juma. Kiongozi anaweza kurudi nyuma na kufanya hadithi ile ile juma linalofuata pamoja na kweli ya kiroho ingine. Kumbuka sio kamwe kupoteza muda kurudi kujifunza Maandiko Matakatifu.

9. Baada ya kusoma hadithi, pitia “kweli za kiroho”. Kila kweli ni dondoo muhimu kabisa la imani, na baadhi inaweza ikawa ni vigumu kuelewa. Chukuwa muda wa kutosha utakaohitajika kurudi kusoma na uruhusu washiriki kuuliza maswali. Usiwe na woga wa maswali, hakuna shida hata kama haujui majibu. Ikiwa mtu Fulani

anauliza swali ambalo wewe haujui jinsi gani ya kulijibu, wewe sema tu “mimi sina uhakika lakini nitatafuta jibu lake au nitamuuliza mchungaji juma hili na nitatoa jibu juma lijalo.”

- Ikiwa kuna majadiliano kuhusu kitu fulani, uwe mwangalifu kutokuruhusu kikundi kupotosha somo. Huenda kukawa na washiriki ambao wataleta hoja ambazo hazihusiani au kujaribu kubadili somo. Kamwe usibishane na mwana kikundi, lakini wewe utahitaji kusema, “mimi ninaheshimu
- maoni yako kuhusu swaki hili, lakini sisi tuko hapa kujifunza yale Biblia inayosema kuhusu _____. Ikiwa wewe ungependa, sisi tungezungumuza hii kwa faragha baada ya masomo.” Kuongoza majadiliano ni jambo gumu kabisa kwa kuongoza masomo ya kikundi.

10. Penye mwisho wa kila fundisho, ni muhimu kuwa na muda wa maombezi. Waombezi wajumbe kushirikisha na kukumbuka kuomba kwa ajili ya mahitaji haya sambamba na mahitaji mengine ambayo wewe unayaelewa.

11. Kuwa imara, usiwe na woga!! MUNGU yuko pamoja na wewe; nayeye anataka kukutumia wewe katika njia maalumu. MUNGU akubariki wewe na familia yako mara wewe unapokubali wajibu huu wa kuwafuata waumini wapya.

- *TAHADHARI, habari zote zilizoandikwa katika serufi ni kwa ajili ya kiongozi tu na haina haja ya kuisoma mbele ya kundi zima.*

- *Maandiko yote ya kibiblia, yamechukuliwa kutoka kwa tafsiri mpya ya King James.*

- *Somo hili linaweza kunukuliwa bure kwa kusudi la kufundisha, lakini kamwe lisiuzwe kwa kutengeneza faida.*

(c) **Junta de Missoes Nacionais, CBB, Rio de Janeiro, RJ.**

KUJA KWA YESU MARA YA KWANZA NA MARA YA PILI

MATHAYO 1 NA 24

SOMO LA 1

"Kesheni basi, kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu …….. kwa sababu hiyo ninyi nanyi jiwekeni tayari;Kwa kuwa katika

saa msiyodhani mwana wa adamu yuaja,"Mathayo 24:42,44.

- *Kama inawezekana ruhusu kila mshiriki wa kikundi ambaye anaweza kuandika alete daftari iliyo wazi na kalamu ya wino kwenye somo hili. ikiwa kundi halijui kusoma na kuandika au wanaweza kusoma na kuandika kwa shida, sehemu hii ya somo haitawezekana, lakini hiyo haina shida.*

Wakati ule Warumi walipokuwa wanatawala ulimwengu uliojulikana,kulikuwa na msichana mdogo bado bikira katika nchi ya Israel jina lake Maria ambaye alikuwa amechumbiwa na wanamume jina lake YusufuSasa,,Maria akawa mja mzito kabla hawajaoana, na wakati yusufu alipogundua hivyo, alitaka kuvunja uchumba wao. Hivyo, usiku mmoja aliazimu lakini kufanya hivyo kwa siri ili asimuaibishe hadhalani Maria.

Alipokuwa anafikiria mambo yote hayo malaika wa Bwana alimjia.Malaika alimwambia Yusufu,kuendelea kumuoa Maria kwa sababu hakumdanganya lakini amebeba mambo kwa uwezo wa roho Mtakatifu. Malaika alimwambia Yusufu kuwa alikuwa Maria azae motto ambaye amekuwa akitabiriwa na manabii wa kale wa kiyahudi. Mtoto ambaye angemzaa angekuwa ni yule aliyetabiriwa na nabii Isaya wakati aliposema "Bikira atachukua mimba naye atamzaa mwana, nao watamwita jina lake Imanuel, yaani "MUNGU PAMOJA NASI."

Hivyo Yusufu akamwamini malaika na akamchukua Maria kuwa mkewe kwa hali yoyote ile, iwapo hawakuwa na uhusiano wowote wa ngono mpaka hapo baada ya kuzaliwa mtoto, Hivyo Yesu alizaliwa na Bikra. Yusufu alimwita mtoto jina, Yesu.

Biblia imefanya tabiri nyingi kuhusu kuja kwa Yesu. Kuzaliwa kwa Yesu kulitabiriwa katika Agano la kale sambamba na majukumu yaliyopelekea kwa kifo chake na ufufuo. Yesu mwenyewe, alifanya ahadi nyingi kuhusu yeye alikuwa nani na atafanya nini Baadhi ya unabii wa Yesu sambamba na unabii mwingine kutokaAgano la kale bado

haujatimilika. Nabii hizi zinatuambia kwamba Yesu atakuja tena duniani. Kuja kwake Yesu mara ya kwanza kulikuwa katika mahali pa unyenyekevu kwa sababu yeye alikuja kama mtumishi atesekaye. Lakini Biblia inatufundisha sisi kwamba kuja kwake mara ya pili kutakuwa tofauti kabisa.

Yesu aliwaambia wafuasi wake juu ya kuja kwake wakati alipowafundi mahali pale palipoitwa mlima wa Mizeituni. Yesu aliwaambia mambo haya alipokuwa akijibu swali la “Na ni nini dalili ya kuja kwako nay a mwisho wa dunia?”

Yesu aliwajibu wafuasi wake kwanza kwa tahadhari, alipowaambia wao kuchukuwa tahadhari kubwa ili kwamba pasiwepo hata mmoja wa kuwadanganya waokwa wao. Yesu alieleza kwamba jinsi gani ya kuja kwake Yeye kunavyokaribia, watu wengi zaidi na zaidi watakuja wakitumia jina lake. Wao

watasema, “mimi ni Kristo” kwa bahati mbaya, watu wengi watawaamini hawa wanabii wa uongo.na kwa wakati vilevile, kutakuwa na vita vingi baina ya watu wa mataifa mbali mbali tofauti ya ulimwengu. Kutakuwa na misiba mine ya kutisha msukosuko na matetesi ya vita, njaa, magonjwa na mitetemeko ya ardhi. Lakini mambo haya ni mwanzo tu. Kwani kutakuwa na masikitiko mengi zaidi ambayo yatakuja kabla ya mwisho kuwadia.

Mwanadamu atamsaliti mwenzake; watauwana wao kwa wao; na watachukiana wao kwa wao sababu ya imani zao katika Kristo. Kutakuwa na manabii wa uongo wengi ambao watazunguka zunguka wakiwadanganya watu. Uvunjaji wa sheria utaongezeka, na upendo ambao watu walikuwa nao kwa mtu na mwingine hapo awali utakuwa baridi. Kupitia mabo yote haya, kwa hali yoyote ile, habari njema ya Kristo itaendelea kushirikishwa mpaka mataifa yote yatakapokuwa yameisha sikia juu ya Kristo na ndipo mwisho utakapokuja.

Kutakuwa na dhiki kubwa au usumbufu katika ulimengu mzima. Na kama Mungu angemwacha mwanadamu aendelee kama anavyopenda, tungekuwa punde tumejiangamiza kabisa sisi wenyewe. Kwa ajili ya wafuasi wa Kristo, kwa hali yoyote ile, Mungu atapunguza siku za taabu na mateso duniani.

Hivyo msiamini manabii wa uongo na Wakristo wa uongo ambao wanakwenda hapa na pale wakifanya dalili nyingi za kuvutia na maajabu. Watu hawa

wanajaribu tu kuwadanganya watu. Hata ikiwezekana wale ambao wameisha yatoa maisha yao kwa Yesu Kristo.

Kisha siku moja, kama umeme unavyokuja kutoka mashariki na kuangaza magharibi vivyo hivyo ndivyo itakavyokuwasiku yakuja kwake Mwana wa Adamu. Baada ya dhiki, juu litatiwa giza, mwezi nao hautatoa mwanga, nyota zitadondoka toka angani na nguvu za mbinguni zitatikisika. Ndipo dalili ya Mwana wa Adamu zitaonekana mbinguni, na ndipo makabila yote ya duniani yataomboleza, na watamwona Mwana wa Adamu akija juu ya mawingu pamoja na uwezo na utukufu mwingi. Na yeye atawatuma malaika wake pamoja na sauti kuu ya tarumbeta, na watawasanya pamoja watu

wote ambao wametoa maisha yao kwa Yesu Kristo. Na hawa watakusanywa kutoka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu mwingine.

Kwa haraka, ni lini hii itatokea, hakuna ajuaye hata mmoja. Malaika wa mbinguni hata nao hawajui ni lini Yesu atakuja tena ulimwenguni. Hakuna hata mmoja ajuaye ni lini Yesu Kristo atarudi duniani ila Baba.

“Kwa sababu hiyo, ninyi nanyi jiwekeni tayari kwa kuwa katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja.

MASWALI YA MDOMO

1. Yesu alizaliwa katika nchi gani?

2. Majina yapi ya wazazi wa kidunia wa Yesu?

3. Ni muujiza upi kuhusu kuja kwake Yesu duniani kwa mara ya kwanza?

4. Nabii Isaya alitabili kwamba Yesu angelizaliwa na Bikra na kuitwa Imanueli yaani “_____
_____
_____.”

5. Wakati Yesu alipokuwa pamoja na wanafunzi wake kwenye mlima wa Mizeituni, ni swali lipi ambalo wanafunzi walimuliza Yesu?

6. Yesu aliwaambia wanafunzi wake wawe waangalifu kiasi kwamba wao wasije kudanganywa na watu wa aina gani?

7. Yesu alisema kuwa watu wengi watakuja wakidai kuwa wao ni nani?

8. Yesu alitaja mambo manne ya kutisha ambayo yatatokea ulimwenguni kote kabla ya yeye kurudi. Mambo haya ni yapi?
   V _____
   N_____
   M_____ na
   W_____.

9. Yesu alisema kwamba wafuasi wake watateseka kwa sababu ya wao kuamini katika Kristo. Ni baadhi ya mambo yapi ambayo Yesu alisema kwamba watu watafanyiana wao kwa wao?

10. Yesu alisema manabii wa uongo wangekuwa na uwezo wa kufanya mambo gani ambayo hata wafuasi wa Yesu wangepumbazwa?

11. Yesu alisema kuja kwake kungekuwa kama tukio lipi katika nguvu za athali?

12. Wakati Yesu atakaporudi ulimwenguni _____ makabila yote ya dunia yatamwona yeye?

13. Kutakuja kutokea nini kwa jua. Kwa mwezi na kwa nyota wakati Yesu atakaporudi tena?

14. Watu wa Mungu watajumuika wapi?

15. Ni nani mmoja pekee ambaye anajua ni lini Yesu Kristo atakuja tena?

16. Jinsi gani nimchukulie mtu fulani ikiwa anafanya miujiza ambayo haimo katika jina la Yesu au anadai kuwa yeye ni Kristo?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 1, 24

SOMO LA 1

1. Jinsi kama Yesu alivyokuja mara ya kwanza katika utimilifu wa unabii, **yeye atakuja tena akiwa na uweza na utukufu mkuu.** Zipo dini nyingi za uongo wengi, na watu wengi wanaodai kuwa Mungu. **Wakati Yesu atakapokuja tena kutakuwa hakuna shaka ya kuhusu yeye ni nani.** Biblia inatufundisha kwamba kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri kwamba yeye ni Bwana. Yeyote anayekuja kwetu sisi na anadai kuwa nabii mpya. Kristo mpya au Mungu ni nabii mwongo na mzushi.

2. **Yeye atawakusanya watu wake wote kutoka mwisho huu wa mbingu ahadi mwisho mwingine.**

- Yesu aliahidi kuja na alikuja. Aliahidi kuja tena na atakuja. Aliahidi kuwakusanya wafuasi wake wote na atawakusanya.

- Wakati tunapomuomba Yesu kuja katika maisha yetu, wakati sisi tunatoa mioyo yetu kwake yeye, Yesu anaahidi kwamba yeye kamwe hatatuacha sisi au kututupa sisi. Hii inamaana kwamba, haimaanishi ikiwa tumetenda dhambi (na sisi sote

tuta) Mungu ni mwaminifu kutunza ahadi zake kwetu sisi. Haidhuru ni kitu gani kinatokea kwetu au tunafanya nini. Ikiwa tumeisha toa maisha yetu kwa Yesu, yeye atakupeleka pamoja naye hadi mbinguni na wakati wa kurudi kwake sisi tutakutana na yeye katika mawingu.

3. **Watu wa Mungu watateseka kwa ajili ya kufuata yeye.**

   Biblia inatuambia kwa jinsi ulimwengu unavyokaribia mwisho, watu watakuwa zaidi na zaidi waovu. Watu watachukia zaidi, watauwa zaidi na wasalitiana kila mtu na mwenzake zaidi. Biblia inasema kwamba watu wengi watachukia wale ambao wanamfuata Yesu na watawatendea vibaya.

   Huenda wewe ulisha wahi kuona watu wakikutendea wewe tofauti kwa sababu ulikata shauri kumfuata Yesu. Kwa mara nyingi, wakati mtu fulani akitoa maisha yake kwa Kristo, familiya yake huwa inashtuka. Mara nyingine familia inachanganyikiwa na wakati mwingine familia huwa haikubali uamuzi huo. Jinsi gani nia za watu kuhusu wewe zilivyobadilika tangu wakati wewe ulipomuomba Yesu kuingia katika moyo wako? Je, unao watu, huenda hata marafiki zako wa karibu na familia. Wamekuumiza wewe au wamekuwa hawakukubali kwa sababu ya uamuzi wako wa kumfuata Kristo?

Biblia inatufundisha kwamba lazima tuwapende watu hata ikiwa hawatutegemezi sisi au hata kutuumiza sisi (Mathayo 5:45-48). Sisi lazima tuwapende na kuomba kwa ajili yao. Hivi ndivyo Yesu alivyowatendea wale waliomuumiza na kumsaliti yeye na kuwa mfuasi wa Kristo ni kufuata mfano wake wa upendo. Biblia pia inatufundisha kwamba kuwa mibaraka maalum iliyohifadhiwa kwa ajili ya kumfuata Kristo. Kwa kweli, Biblia inatuambi sisi kuhesabu yote kuwa ni furaha kwa sababu siku moja itakuwa inahesabiwa kuwa na thamani ya gharama tuliyoilipa.

- Ikiwa unajisikia kufarijika, shirikisha udhoefu wako juu ya yale yaliyotokea kwao tangia wakati ule ulipompokea Krsito. Je, familia yako imekuwa tegemezi? Je, wewe nini muumini peke yako katika familia? Je, familia yako inaelewa unachokifanya ni nini? Je, kuna yeyote anayeteseka kutokana na wewe kumpokea Kristo? Ikiwa mojawapo analo tatizo, Ebu sote tukumbuke kuomba kwa ajili ya mtu huyu kama kikundi.

- Lakini kabla ya sisi kuomba, ebu kila mtu ambaye alileta daftari au wale ambao wanazo karatasi na karamu za wino wazitoe. Ikiwa wewe unalo daftari, andika majina ya kila mjumbe wa kikundi juu ya karatasi pekee. Chini ya kila jina, sisi

Tutaorodhesha mahitaji ya maombi ya kila mtu. Ebu sisi vile vile tufanye orodha ya watu tunaowaelewa wanaohitaji kumpokea Yesu, kama vile wana familia wengine na marafiki. Shirikiana na orodha hizi pamoja kila mtu na mwenzake ili kwamba sisi tunaweza kujiunga na marafiki zetu katika mapambano kwa ajili ya marafiki zetu na wapenzi wetu.

- Wakati tunapokwenda nje juma hili, ebu tukubaliane kuombeana. Kila mtu na mwingine kila siku. Weka daftari hili au kipande cha karatasi katika chumba chako cha kulala, na kabla yaw ewe kwenda kulala au wakati wewe unapoamka, ichukue na ukumbuke kuombea mwingine.

- Ebu sisi tumalize mkutano huu kwa kumshukuru Mungu kwa kuwa mwaminifu wa kutunza ahadi zake. Ebu na tumushukuru kwasababu ya kuja kwake ulimwenguni kwa mara ya kwanza kutuokoa sisi kutoka kwa dhambi zetu, na kwa ajili ya ahadi ya kuja kwake mara ya pili.

- Ebu sisi tuombe atusaidie sisi kuwa waaminifu kuomba kwa ajili ya kila mtu na mwenzake kila siku kwa juma linalofuata. Mwishowe ebu tuombe maombi rasmi kwa ajili ya yeyote ambaye ana wakati mgumu kwa sababu ya uamuzi wao wa kumfuata Kristo.

YESU ANAKIMBILIA MISRI NA UBATIZO WAKE

MATHAYO 2-3

SOMO LA 2

"Naye Yesu alipokwisha batizwa, mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake. Na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye." Mathayo 3:16-17

MARUDIO:

1. Jina la mama yake Yesu lilikuwa _____.

2. Nabii Isaya alisema kwamba Yesu angeitwa Imanueli ambayo maana yake ni “Mungu _____ _____.”

3. Penye mlima wa Mizeituni wakati wanafunzi walipomuuliza yesu kurudi kwake ulimwenguni, Yesu alisema wanafunzi wake lazima wawe waangalifu ili kwamba wasije wakandanganywa na manabii wa _____.

4. Yesu alisema wengi watakuja wakidai kuwa ni _____.

5. Yesu alisema kwamba mambo ya kutisha yangetokea ulimwenguni kama vile
   V_____,
   N_____,
   M_____na
   W_____.

6. Yesu alisema kuwa wafuasi wa Kristo wangeteseka pia; kwa nini?

7. Yesu alisema kuja kwake kungekuwa kama kitu gani cha asili?

8. Je, itawezekana “kukosa kuona” kurudi kwake Yesu?

9. Ni nani mmoja pekee anayejua ni lini Yesu Kristo atakuja tena?

10. Jinsi gani mimi nimchukulie mtu fulani anayefanya miujiza ambayo haimo katika jina ka Yesu?

11. Mimi nijihesabu vipi mwenyewe _____ wakati mtu mmoja ananifanyia vituko kwa sababu ya Kristo?

12. Ninapashwa kuwatendea wale ambao wanitenda vibaya kwa sababu ya Kristo kwa _____.

    Yesu alizaliwa katika Bedhelehemu na akakaa huko mpaka wakati yeye alipotembelewa na mamajusi toka mashariki. Watu hawa walikuja, katika Israeli wakiifuata ile nyota iliyokuwa inang’aa. Kuingia katika mkoa wa Wayahudi wa Yuda, kwanza wao walikwenda kwa mji mkuu wa Yerusalemu. Huko walikwenda kwa Mfalme Herode na wakamuuliza ni wapi mfalme mpya wa Israeli alikozaliwa kwani wao wameiona nyota yake.

    Herode na wote wa Yerusalemu pamoja naye walisumbuka wakati waliposikia mambo haya. Hivyo aliitisha mkutano wa siri wa viongozi wa dini wote. Aliwauliza wasomi ni wapi Maandiko

Matakatifu yaliposema yule Mfalme aliyeahidiwa wa

wayahudi angezaliwa. Mamajusi walimwambia Herode kwamba unabii ulitaja kwamba mtoto angezaliwa katika Bethrehemu.

Herode aliwaambia mamajusi mahali pa kwenda. Lakini kabla hawajaondoka makao yake, yeye aliwauliza wao ni lini hakika walipoiona kwa mara ya kwanza hiyo nyota. Herode alifanya hivi ili aweze kupata umri wa mtoto.

Mamajusi waliendelea na safari yao hadi Bethrehemu, na nyota ikiwaongoza wao hadi kwenye mahali Yesu alipokuwa anaishi, Mamajusi waliingia mahali pale na wakamsujudia Yesu. Wao wakampelekea zawadi za thamani; dhahabu, uvumba na manemane. Kabla hawajaondoka kurudi nyumbani, watu hawa walikuwa na ndoto kutoka kwa Mungu. Katika ndoto hii waliambiwa wasije wakarudi nyumbani kwa njia ya yelusalem,jinsi kama Herode alivyowaambia.walikwenda zao nyumbani kwa njia nyingine.

Yusufu vile vile alikuwa na ndoto nyingine kutoka kwa bwana.ndoto hii ilimuonya yusufu kuondoka mara moja pamoja na maria na mtoto.ilibidi waende hadi misri na kukaa huko mpaka atakapo sikia neno kutoka kwa bwana.yusufu aliambiwa kwamba herode

alikuwa anaenda kujaribu kumuua mtoto.hii ingekuwa ni katika utimilifu wa unabii wa agano la kale kutoka misri nilimuita mwangu.

Herode hakika alipanga kumuua mtoto aliyeahidiwa.aliwauwa watoto wa kiume waliokuwa wametimiza umriwa miaka miwili na chini yake ambao walikuwa katika bethelehemu au katika maeneo yaliyo zungukwa na bethelehemu.

Baada ya kifo cha herode,yusufu alikuwa na ndoto nyingine ikimshauri kurudi hadi islaeli.yusufu alimtii mungu.alikwenda kwa mkoa wa kaskazini ulioitwa galilaya,na wao wakaishi katika mji wa nazaleti

Sasa,katika siku hizo,kulikuwa na mtu mmoja aliyeitwa yohana mbatizaji ambaye alikujaakihubiri katika nyikani mwa uyahudi.alihubili ujumbe,tubuni kwa maana ufalume wa mungu umekaribia.yohana mwenyewe alivaa nguo za singa za ngamia pamoja na mkanda wa ngozi kiunonimwake.chakula chake kilikuwa ni nzinge na asali ya mwitu.

Yerusalemu na yuda yote na nchi zote kando kando ya yordani walitoka nje na kwenda kwake na walibatizwa katika yordani,huku wakiziungama dhambi zao. vile vile,wengi wa viongozi wa dini,mafarisayo na masadukaya walikuwa wakija kusikilza yohana

anayoyasema.yohana aliwaita watu hawa wazao wa nyoka kwa sababu wao waliweka imani ya urithi na mapokeo ya dini yao kuwaokoa wao,pasipo kuamini kwamba wanalazimika kutubu dhambi zao.

Wakati yohana mbatizaji alipokuwa akihubiri alizungumzia juu ya mmoja ambaye alikuwa anakuja ambaye angewabatiza kwa roho mtakatifu na moto.yohana alisema

kwamba,huyu alikuwa anakwenda kuwagawa watu,atawakusanya kwake wale ambao wanaoweka imani yao katika yeye na kuwaacha waliobakia kuungua kwa moto usiozimika.

Kasha yesu alikuja kutoka galilaya hadi yordani kwa yohana ili abatizwe na yohana.Yohana alijaribu kumzuia,kwani alijisikia kwamba hastahili kumbatiza yesu.lakini yesu akakazia kubatizwa kwa sababu alitaka haki yote kutimilika.mara yesu alipokwisha kubatizwa,mara moja akapanda kutoka majini,na kila mmoja angeweza kuona mbingu zikimfunukia.roho mtakatifu kisha akatua mbinguni,akisema huyu ni mwanangu,mpendwa wangu,ninayependezwa naye.

MASWALI YA MDOMO

1. ni watu wa aina gani waliokuja kumtembelea yesu kutoka mashariki na walimtolea vitu gani?

2. ni katika njia gani watu hawa walisimama kwanza,na walizungumza na nani?

3. ni kwanini mungu alimuonya yusufu kukimbilia misri?na yusufu alijuaje ni wakati gani ulikuwa wa salama kurudi?

4. yohana mbatizaji alihubiri wapi?

5. alikuwa anaonekanaje?

6. ni nini uliokuwa ujumbe wake kwa watu?

7. kulitokea nini kwa watu ambao walitubu dhambi zao?

8. ni kwa nini yohana mbatizaji aliwaita mafarisayo na masandukayo uzao wa nyoka?

9. yohana alihubili juu ya mmoja ajaye ambaye alikuwa mkubwa kuliko yeye.alisema huyu angewagawanya watu wa ulimwengu.Yohana alisema kwamba wale wanaoweka imani zao katika huyo wangeokolewa lakini walio salia wangeungua na moto

10. ni nani aliyekuja kutoka galilaya ili abatizwe na yohana?

11. yesu alikazia kwamba yohana abatizwe hata kama alijisikia alistahili.ni nini iliyo kuwa sababu ambayo aliitoa?

12. kulitokea nini wakati yesu alipopanda juu kutoka majini?

KWELI ZA KIROHO

MATHAYO 2-3

SOMO LA 2

1. **Sisi tunaweza kuona ubora wa Mungu kwa ajili ya maisha yetu wakati tunapomtii yeye kikamilifu.** Mungu alimwambia Yusufu kufanya mambo mengi sana ambayo yeye vinginevyo asingeweza kuvifanya. Yusufu alimtii Mungu na akamuoa Maria hata ingawa alikuwa mjamzito. Yusufu alimtumaini Mungu, hata hivyo mimba ya Maria ilikuwa kitu kisichowezekana kueleweka kwa Yusufu. kiasha tena baada ya kuishi katika Bethlehemu, Mungu aliwaambia wao kuhama hadi Misiri.

   Misiri ilikuwa ni nchi ya Kigeni, mahali walizungumza lugha ya kigeni na wakaishi tofauti kabisa kuabudu miungu ya uongo. Hatua hii haikuwa rahisi kwa mtu na mkewe na mtoto mdogo. Kwa hali yoyote ile, Yusufu alichagua kutii na kama matokeo, maisha ya Yesu yalisalimika.

   Jinsi kama Mungu alivyokuwa na mpango maalumu kwa ajili ya maisha ya Yusufu, Mungu ana mpango maalum uliobinafsishwa kwa kila mmoja wetu. Biblia inasema kwamba tangia wakati tulipokuwa bado tungali katika matumbo ya mama zetu, Mungu tayari aliisha tujua sisi na alituumba sisi kwa kusudi maalum. Ikiwa sisi tunataka

kuona ubora kwa ajili ya maisha yetu na maisha ya watoto wetu, lazima sisi tutii kwa uangalifu maagizo yake kwetu. Biblia inasema, Mungu anashauku kusema na kila mmoja wetu katika mioyo yetu jinsi sisi tunavyoomba na kusoma Neno lake. Mungu anatuongoza sisi kwa maisha yenye kujaa na maisha tele pamoja na yeye. Safari nyingi Mungu anazungumuza moja kwa moja kwetu sisi wakati tunapoomba na kusoma Neno lake. Anashughulika na sisi kuhusu hali dhahiri na maamuzi dhahiri tunayopashwa kufanya. Sisi tunahitaji kufanya chaguo hivi sasa kabla sisi hatujawa na chaguo kwamba wakati wa nyakati ngumu inapowadia; tutafanya kama Yusufu alivyofanya, uamuzi wa kumtii Mungu, bila kujali ni nini. Hata ikiwa wakati Fulani tungefanya kitu kingine.

Kwa mfano, mimi ninaye rafiki toka chuoni ambaye ni mzuri na anazo akili. Dada huyu anampenda Mungu, lakini pia anataka sana kuolewa. Aliwapanga wanaume wengi, lakini uhusiano wao haukutekelezeka. Hivyo siku moja, jamaa mmoja akaja katika maisha yake ambaye alikuwa ana umbo zuri, ana akili, mcheshi na hata tajiri. Yule jamaa alikuwa ni kila kitu ambacho yule dada alikuwa kamwe hajawahi kukitazamia kutoka mwanaume. Alikuwa na kasoro moja – yule mwanamume hakuwa na uhusiano mzuri na Mungu. Rafiki yangu alijua kwamba Mungu hataki sisi tuoane na watu au hata kuahidiana na watu

ambao hawampendi Mungu, lakini huu uamuzi kwa wakati ule ulikuwa vigumu kwake. Hakika dada

yule alitaka kuolewa. Ilivyoonekana ni kwamba wote marafiki zake walikuwa tayari wameishapata wanaume; na mbali na hayo, yule mwanaume alikuwa amependezwa sana na yule dada. Kwa bahati mbaya, alikuwa hajafanya uamuzi wa kumtii Kristo na asiahidiane na wasio amini, hivyo uhusiano ukawa mzito zaidi na ilibidi afanye uamuzi kuhusu ndoa. Hakuwa na nguvu tosha za kumfuata Yesu achilia mbali gharama, kama Yusufu alivyofanya. Kwa hiyo dada alifanya uamuzi usio sahihi na wakaoana na mwanaume asiye sahihi, na leo hii bado anateseka kwa matokeo kutokana na uamuzi huu mbaya.

- Je, Mungu anasema nawe kuhusu kitu Fulani dhahiri katika maisha yako? Mungu anakuuliza wewe kubali kitu Fulani katika maisha yako. Ni vigumu kwako wewe kubadilika? Kama ni hivyo na ukiwa ni wewe unajisikia faraja (tafadhari usishirikishe mambo ambayo yatakufanya wewe usifarijike baadaye) shirikisha hii pamoja na kikundi. Kila mtu anapashwa hapo kuandika hitaji hili chini ya jina lako katika daftari yake ya maombi – ili kukumbukwa na kuombewa kila siku wakati wa juma lijalo. Mungu anashauku

na atakupa wewe nguvu ya kutii mipango yake kwa ajili ya maisha yako.

2. Kabla ya Yesu kwenda tena mbinguni, baada ya ufufuo wake, yeye alitupatia sisi zote, wafuasi wake, amri. Ebu sisi turudie maneno ya mwisho ya Yesu kabla ya yeye kurudia huko mbinguni, "*Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, la Mwana na la Roho Mtakatifu na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari."* Baadaye katika somo hili, sisi tutajifunza jinsi gani ya kwenda na kuwaambia wengine kuhusu Yesu. Ipo amri moja sisi sote lazima tuifanye sisiwenyewe katika kutii maneno ya Bwana. Sisi ni lazima tubatizwe katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu.

- Ubatizo ni tendo la kawaida la utiifu tuliopewa sisi na Kristo. Muumini aliyekomaa zaidi katika Kristo kawaida humchovya na kasha kumuinua juu muumini mpya kutoka majina kama mfano wa kifo, kuzikwa na ufufuo wa Kristo. Ubatizo sio utaratibu wa dini ambao unakutambulisha wewe kwa dini dhahiri au dhehebu. Sio tendo la kiroho ambalo hukusafisha moyo wa dhambi, ni mfano, maonyesho ya hadhara juu ya nadhiri zetu kwa kumfuata Yesu.

- Yesu hakubatizwa kama mtoto mchanga. Katika Injili ya Luka, sisi tunajifunza kwamba Yesu alichukuliwa hekaluni akiwa mtoto mchanga. Hapo kuhani alimbariki yeye na wazazi wake. Hii haikuwa ubatizo.

- Ubatizo wa Yesu ulikuwa chaguo ambalo Yesualilifanya yeye mwenyewe. Katika mfano wa Kristo, sisi sote tunapaswa kwenda, sisi wenyewe na kutafuta kubatizwa na mtu wa Mungu.

- Je, unafikiria nini juu ya ubatizo? Je, unafikiria kuwa ni kitu kigumu kubatizwa katika mfano wa Kristo? Je, wewe unahitaji kubatizwa? Familia yako ingefikiria nini ikiwa wewe utabatizwa? Je, wewe ungependa kubatizwa?

KUJARIBIWA KWA YESU
MATHAYO 4

SOMO LA 3

"Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu" Mathayo 4:4.

- Kiongozi – Kumbuka, ikiwa kuna wajumbe katika kikundi chako ambao hawajui kusoma na kuandika au wanajua kidogo. Wewe lazima uwe mwepesi kuhisi na utahitaji kuiga kanuni katika fundisho hili kwa utangulizi wao.

MARUDIO:-

1. Nabii Isaya alisema Yesu angeitwa Imanueli ambalo linatafsiriwa kuwa maana ya Mungu _____.

2. Yesu alisema kwamba wakati yeye atakaporudi kwa mara ya mwisho ulimwenguni itakuwa kama ghafla ya _____

3. Yesu alisema kwamba wakati yeye atakaporudi kwa ulimwengu, hakuna hata mmoja atakayechanganyikiwa juu ya nani hasa Kristo wa kweli _____ watamwona yeye akija juu ya mawingu pamoja na nguvu na utukufu mkuu.

4. Yesu alisema kuwa kabla hajawahi yeye, wengi watafanya tamasha za hila wakijifanya kuwa Kristo. Lazima sisi tuwe waangalifu sana kiasi kwamba _____ na hawa manabii wa uongo.

5. Yesu alisema sisi tunapashwa kujiona wenye _____ wakati watu watakapo tuudhi sisi kwa sababu ya Yesu Kristo. Alisema kuwatendea hawa watu kwa _____

6. Yesu alisema yule mmoja pekee anayejua atarudi lini ulimwenguni ni _____

7. Mtu anayeishi nyikani jina lake _____ alihubiri ujumbe wa kutubu, alivaa ngozi za ngamia na kula nyingi.

8. Wengi walikuja ili wabatizwe na Yohana na walitibu _____ zao.

9. Yohana alisema kwamba mmoja yuaja ambaye wagawa watu wa ulimwengu na kwamba wale ambao walimkataa yeye wangehukumiwa kwa _____ usiozimika.

10. Penye ubatizo wa Yesu _____ alishuka chini kama hua na _____ ikasikika kutoka mbinguni.

11. Katika maneno ya mwisho ya Yesu kabla ya kwenda kurudi mbinguni, aliwaambia wanafunzi wake kuwa _____ kila mmoja ambaye atampokea Kristo kama Bwana.

12. Sisi lazima tu _____ sio kwa sababu inatusafisha sisi kwa dhambi zetu, lakini kwa sababu ni mfano ambao unatutambulisha sisi na _____

13. Ubatizo ni mfano wa _____ kuzikwa na _____ kwa Yesu.

Baada ya ubatizo wa Yesu, Roho mtakatifu alimuongoza Yesu kwenda nyikani ili ajaribiwe na Shetani. Yesu alikaa huko siku arobaini mchana na usiku akiwa amefunga. Baada ya siku hizi arobaini, Yesu aliona njaa. Ilikuwa ndio wakati huo ambao Shetani alimjia Yesu na kumwambia, "Ukiwa ndiwe mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate." Yesu alimjibu Shetani kwa kutumia kifungu kinachopatikana katika Agano la la kale kinachosema, "*Mutu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."*

Baadaye ibilisi akamuchukua mpaka katika Yerusalemu, mji mkuu. Pale Ibilisi akamwambia Yesu, "Ukiwa ndiwe mwana wa Mungu, jitupe chini. Kwa maana imeandikwa; atakuagizia malaika wake na mikononi mwake watakuchukua usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe. "Yesu akamjibu tena akitumia maneno kutoka Biblia yanayosema, "Usimjaribu Bwana Mungu wako."

Tena, Ibilisi akamchukua Yesu, safari hii kwenye mlima mrefu mno. Kutoka mahali hapo, wote wawili waliweza kutazama milki zote za ulimwengu na fahari zake. Shetani akamwambia Yesu, " Haya yote nitakupa wewe ikiwa wewe utaniangukia chini na kunisujudia mimi." Yesu alijibu kwa kusema, "Nenda zako Shetani! Kwa

maana imeandikwa, “Musujudie Bwana Mungu wako umwabudu yeye peke yake.” Shetani alitii amri ya Yesu na akamwacha. Ndipo wakaja malaika na wakamtumikia Yesu.

MASWALI YA MDOMO

1. Ni wapi ambapo Roho Mtakatifu alimpeleka Yesu akajaribiwe?

2. Yesu kwa muda wa siku arobaini alifanya bila nini kabla ya Shetani kumjaribu?

3. Katika majaribu mawili ya mwanzo, Shetani alitoa changa moto kwa Yesu kuthibitisha kwamba yeye ni nani?

4. Katika jaribu la kwanza ni katika nini Shetani alijaribu kumpata Yesu ili ageuze mawe?

5. Jinsi gani Yesu alimudu Shetani katika jaribu la kwanza?

6. Katika jaribu la pili, Shetani alijaribu kumpata Yesu afanye nini wakati walipompeleka, juu ya kilele cha hekalu katika Yerusalemu?

7. Jinsi gani Yesu alipomshinda Shetani katika jaribu la pili?

8. Katika jaribu la tatu, Shetani aliahidi kumpatia Yesu milki zote za ulimwengu ikiwa Yesu angalifanya kitu kimoja tu. Ni kitu gani Shetani alichotaka Yesu akifanye?

9. Jinsi gani Yesu alivyomshinda Shetani katika jaribu la tatu?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 4

SOMO LA 3

1. **Sisi tutapata majaribu hata baada ya kutoa maisha yetu kwa Kristo.** Hata kama Yesu alikabili majaribu, sisi pia tunakabiliana na majaribu. Biblia inatufundisha sisi kwamba tunajaribiwa sio tu na Shetani, lakini mara nyingi zaidi na tamaa zetu wenyewe (Yakobo 1:14). Biblia inatufundisha sisi kwamba kuna mapambano makubwa katika ndani ya kila moja ya mioyo yetu kati ya shauku zetu za kutenda mema na shauku zetu za kutenda maovu, "maana sijui nilifanyalo, kwa sababu lile nilipendalo, silitendi, bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda …….. kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi, bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo." (Warumi 7:15, 19).

2. **Wewe utapatwa na majaribu kwa sababu wewe hivi sasa unazo asili mbili ndani yako.** Moyo ni roho wa kimwili na ingine ni Roho wa Mungu (Roho Mtakatifu) ndani yako. Wagalatia 5:16-17 inasema, "Basi nasema, enendeni kwa Roho wala hamtatimiza kwamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani kushindana na Roho na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana hata hamuwezi kufanya mnayoyataka; Kutokuwa na mapambano yakila siku kati ya utashi wako dhidi ya mapenzi ya Mungu katika vyote, makubwa na madogo ya maisha."

3. **Sisi tunaweza kushinda majaribu kwa njia ile ile Yesu aliyofanya, kupitia kwa uwezo**

wa Neno la Mungu – Biblia. Waebrania 4:12 inasema, “Maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na Roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Soma mstari huu zaidi ya mara moja. Waulize wajumbe kukuambia wewe, wanafikiri nini, maana ya huu mstari.

Katika mstari huu, ni kifaa gani kilicholinganishwa na Neno la Mungu Je neno la Mungu linaweza kufanya nini?

Neno la Mungu sio tu kitabu cha ushauri. Ni maneno yaliyo hai ambayo Mungu anayotumia kusema kwa kila moja ya yetu katika njia ya kila mmoja peke yake. Linapenya ndani katika sehemu za roho zetu ambao ni Mungu pekee ndiye anayejua.

Kitu kimoja cha muhimu sana ambacho kila mfuasi wa Kristo akifanye ni kutumia muda kila siku peke yake pamoja na Baba. Shetani atafanya kila kitu anachoweza kukuweka wewe mbali na Neno la Mungu kwa sababu Shetani anajua kwamba Neno la Mungu ndilo chanzo chetu cha nguvu. Shetani atatuambia sisi kuwa tunaokazi nyingi, tuna usingizi mzito, sisi tuliisha fanya masomo ya Biblia, Bibulia ni ngumu mno kuielewa, sababu zingine nyingi

kama milioni moja. Sisi lazima tuyatambue mawazo haya kwani ni uongo. Sisi ni lazima tuipe kipaumbele kutumia muda ***kila siku*** katika maombi na katika Neno la Mungu.

Hapa upo mpango rahisi kufuata:

1. Anza na muda wako wa pekee pamoja na Baba ukimuambia ni jinsi gani wewe unavyompenda na umtukuze Yeye kwa ajili ya mambo ya kustaajabu ambayo yeye alivyo.

2. Umshukuru yeye kwa mambo aliyokufanyia katika maisha yako, au majibu kwa maombi ambayo wewe umeisha pokea.

- Ni wazo zuri kutengeneza ukurasa au kutenga sehemu katika daftari yako ya maombi inayoitwa "Asante" na unukuru yale mambo ambayo Mungu anayatenda katika maisha yako, kila mara usisahau tarehe. Kwa njia hii wewe unaweza kutunza kumbukumbu ya jinsi gani Mungu anavyofanya kazi katika maisha yako. (***kumbuka ikiwa washiriki hawawezi kuandika, sehemu hii inahitaji kurukwa***).

3. ombi kwa ajili yawengine: watu wako walio katika masomo ya Biblia, familia yako, marafiki zako, hususani wale ambao hawajamujua Kristo bado, na mahitaji maalum. Ikiwa wewe unao watu wengi wa kuombea, huenda ukahitaji kutanga ukurasa au sehemu kwa kila siku ya juma na gawanya

familia yako na marafiki ukiombea kila mmoja wao kwa jina mara moja kwa juma. (*Hata ikiwa mtu hawezi kusoma na kuandika, ni muhimu kwamba aanze zoezi la kuombea wengine.*)

Kwa mfano:

Jumatatu	**Jumanne**
Shangazi Pam	Bibi
Mjomba Daudi	Mama
Raheli	Papa
Yohana Daudi	Mchungaji Marceli

- Inaweza kuwa ya manufaa kusimama na kufanya hii, sasa hivi pamoja. Ili kwamba kila mmoja anaweza kuanza muda wake wa maombi pasipokuwa kufanya zoezi hili.

4. Soma na utafakari juu ya Neno la Mungu. Biblia inatufundisha sisi kwamba sisi tunapashwa sio tu kusoma Biblia kama vile tunavyosoma kitu kingine chochote, lakini tunapaswa kutafakari juu yake. Hii ina maana sisi tunapashwa:

- Kusoma Biblia taratibu. Ikiwa wewe huwezi kusoma, muombe mtu Fulani aliyekaribu nawe ili akusomee.

- Soma tena na tena mara nyingi ukifikiria kwa undani juu ya maana ya maneno. Inaweza

kuchukua safari nyingi za kusoma kabla hujakaza fikira juu ya ukweli ambao Mungu anajaribu kutuwasilishia.

- Ikiwa inaweza kufanyika, weka jina lako katika ile kweli ya neno jinsi inavyotumiwa. Kwa mfano, ikiwa mstari unasema, “Mheshimu Baba yako na mama yako” Unajielekeza kwako ina maana “Christy, wewe lazima umheshimu baba yako na mama yako.”

- Ombi mstari huu rejeza kwa Mungu na umshukuru Mungu kwa baraka zake na umuombe yeye kwa ajili ya mahitaji maalum. Kwa mfano, “Asante Mungu kwa ajili ya baba yangu wa mbinguni anayekidhi mahitaji yangu ya kila siku, na ambaye yuko pale wakati baba yangu wa duniani hayupo.”

  Biblia inazo kweli za kiroho nyingi ambazo Mungu anataka kuziwasilisha kwetu kuhusu maisha yetu sasa hivi. Hapa kuna mfano wa jinsi gani ya kutafakari juu ya Neno la Mungu.

- Ebu tuanze na sura baada ya ile moja tuliojadiliana leo, Mathayo 5. Ebu tusimame na kila mtu apate muda wa kusoma ile mistari mitatu au minne ya kwanza. Ikiwa kuna mtu hawezi kusoma. Kiongozi anapashwa kusoma mistari hii kwa mtu huyu safari nyingi pasipo maelezo yoyote.

- Sasa, ebu kila mmoja ajaribu kuelewa maana ya mistari na ikiwa tunaweza, ebu tuweke majina yetu katika mistari.

  Usiwe na hofu ya kuruhusu Roho wa Mungu kusema nawe. Hapa kuna mfano: lakini bila shaka sio njia pekee mstari huu unaweza ukatumika katika maisha ya mtu. Haya ni maneno ambayo Bwana aliyasema kwa mtu mmoja alipokuwa akisoma mistari hii.

  Mstari wa 3: *"Heri walio maskini war oho maana ufalme wa mbinguni ni wao."*

  (Mfano wa "ukweli wa kiroho") Mstari 3 – mimi ninayo heri ikiwa niko maskini katika roho kwa kuwa nitaurithi ufalme wa Mungu. Bwana nisaidie mimi kuwa maskini katika roho. Mimi sitaki kuwa na kiburi, majivuno na kujawa na roho yangu. Ahsante Bwana, kwa ajili ya kazi unayoifanya ndani ya maisha yangu. Ahsante Bwana, kwani ninajua kwamba mimi nitaurithi ufalme wa Mungu. Mimi hakika ni mtu aliye barikiwa.

  Mstari 4: "Heri wenye huzuni, maana hao watafarijika."

  (Mfano wa "ukweli wa kiroho") Mstari 4 – "Inakuwa vigumu kwangu kufikiria kuwa mimi nimebarikiwa wakati wa huzuni; kwani kuhuzunika ni wakati wa masikitiko. Lakini

kama mfuasi wa Kristo, mimi ninashukuru kwa sababu mimi ninajua kwamba kwa kweli mimi nimebarikiwa. Kwa kuwa tunalo tumaini kwa ajili yetu ambao tunayo imani katika Kristo. Mungu anatupatia sisi matumaini nahii kwa kweli ni faraja. **Bwana,** ahsante kwa ajili ya kuwa mfariji kwangu wakati mimi ninapopatwa na huzuni katika maisha yangu binafsi wakati wa masikitiko. Ahsante kwa ajili ya faraja mimi niliyoipokea kutoka kwa Roho Mtakatifu katika roho yangu. Ndio Bwana, mimi ninaweza kuona kwamba kama kuwa wewe unanitunza mimi."

Hakuna utaratibu maalum, hakuna maneno au mtindo wowote maalum. Ni muhimu tu kutafakari juu ya maneno ya Mungu. Yaruhusu yalowe kwa kini ya ndani ya roho yako. Wakati yatakapopenyeza katika maisha yako, Mungu atasema pale kwa sehemu zako za ndani kabisa.

Kwa kutumia muda kutafakari juu ya Neno katika njia ya binafsi na kwa msingi wa kudumu, tunakuwa zaidi kama Kristo katika sura zote za maisha yetu. Sio tu kwamba tutaweza kushinda majaribu, lakini tunaonyesha zaidi upendo wa kutenda zaidi mapenzi ya Mungu katika kila njia. Kumjua Mungu katika njia ya binafsi ndio ufunguo kwa maisha ya Kikristo yaliyo na ushindi na

kutafakari juu ya Neno la Mungu ufunguo kwa kumjua Mungu.

- Ikiwa wewe unaweza, gawanya sehemu ya mwisho katika daftari yako ya maombi katika eneo maalum kwa ajili ya kutafakari. Andika tarehe ndani ya kila siku wewe unapofungua Biblia yako, na unukuru angalau ukweli mmoja ambao Mungu yumo anasema kwako. Wakati mwingine ni rahisi zaidi kutafakari juu ya Neno ikiwa wewe unaandika chini mawazo yako, au inaweza kuwa vizuri kwa kurudi nyuma baadaye na kusoma mambo ya thamani Bwana anasema katika moyo wako. Hii ni nafsi ya faragha sana na wakati wa thamanisana katikati yako na Bwana wako.

- Jipe changamoto mwenyewe ya kufanya nadhiri kwako mwenyewe na kwa kikundi chako kwamba kwa juma mojo,wewe utakuwa mwaminifu kutumia angalao dakika kumi na tano pamoja na baba kila sikuikiwa itawezekana andika chini kitu kimoja kwa siku ambacho bwana alicho sema kwako kina husu

nini.ikiwa wewe hauwezi kusoma,ona ikiwa wewe unaweza kumpata mtu mmoja kukusomea wewe huenda kwa dakika chache kwa siku,hili juma lijalo na uone ni kipi kitatokea wakati unaporuhusu neno la mungu kupenyeza ndani ya moyo wako kila siku.

- Ebu sisi sote tuendelee kusoma sura hii ambayo tumeianza(mathayo5).hakuna haraka kumaliza sura hii kwa siku moja.wakti unapo maliza sura,endelea tu kwa sura inayofuata na kisha nyingine.juma lijalo ebu sisi sote turudi na kushirikiana chochote kile ambacho huenda ulikiona wakati wa kutafakari juu ya Neon la mungu.

KUONDOLEWA WOGA KATIKA WAVUVI WA WATU

MATHAYO

SOMO LA 4

"Akamwambia, mbona mmekuwa waoga, enyi wa imani haba? Mara akaondoka akazikemea pepo na bahari, kukawa shwari kuu" Mathayo 8:26.

- Kama kiongozi, kumbuka kuwauliza wana – kikundi ikiwa wanaweza kusoma Biblia zao na kuomba kila siku. Mpatie kila mtu nafasi kushiriki uzoefu. Himiza jitihada zao.

- Pia kwa sababu ya asili ya masomo ya juma hili. Ni muhimu kwa kikundi kuwa na muda wao wa mahitaji ya maombi na kuombeana wakati wa mwanzo wa somo baada ya mwisho. Fanya hili sasa kabla ya kuanza hadithi.

MARUDIO:

1. Nabii Isaya alisema kwamba Yesu angeitwa Imanueli ambayo inatafsiriwa, "Mungu _____ _____."

2. Penye mlima wa Mizeituni wakati Yesu alipokuwa anafundisha wanafunzi wake kuhusu kuja kwake kwa mara ya pili, Yeye aliwaambia kuwa waangalifu kiasi kwamba wasi _____ na manabii wa uongo au watu wanaodai kuwa Kristo hata ikiwa wao wataweza kufanya tamasha za hila.

3. Yesu alisema kwamba atakapokuja mara ya mwisho duniani _____ watamwona akija katika mawingu pamoja na uwezo mkuu na utukufu.

4. Yesu alisema mmoja pekee ambaye anajua ni lini atarudi duniani ni nani _____.

5. Yohana Mbatizaji alibatiza wengi huko nyikani ambao walitubu _____ zao.

6. Kabla ya Yesu kupaa mbinguni, aliwaamuru kwamba wanafunzi wake wote _____ kama Yesu alivyo na Yohana Mbatizaji.

7. Yohana alisema kwamba mmoja alikuwa anakuja ambaye angewagawa watu wa ulimwengu na kwamba wale ambao waliomkataa wangehukumiwa kwa _____ usiozimika.

8. Katika majarida mawili ya mwanzo, Shetani alijaribu kumpa Yesu afanye viini macho ambavyo vingedhihirisha kwamba Yesu ni _____.

9. Katika jaribu la tatu, Shetani alimwambia Yesu kuanguka chini na _____ yeye.

10. Yesu alimjibu ibilisi mara tatu akitumia _____ la _____.

11. Ikiwa tunataka kumjua Mungu vizuri zaidi ni muhimu tuwe tunatumia _____ pamoja na Yeye kila siku.

12. Ni zipi asili mbili zilizomo ndani yako ambazo zinagongana kila moja na nyingine? Roho ya mwili na Roho wa _____.

13. Ikiwa sisi tunataka kushinda majaribu ni muhimu kwamba sisi tunatumia muda wa peke yetu na Mungu _____.

14. Ikiwa sisi tunataka kuwa zaidi kama Yesu, ni muhimu kwamba sisi tunatumia muda wa peke yetu na Mungu _____.

Yesu alianza huduma yake kwa umma baada ya yeye kurudi kutoka nyikani. Yeye alikaa katika eneo kando kando ya Bahari ya Galilaya na akajizatiti mwenyewe nje ya mji wa Kaperanaumu. Yesu alihubiri katika eneo hili ujumbe ule ule ambao ulihubiriwa na Yohana Mbatizaji, "*Tubuni kwa maana ufalme wa Mungu umekaribia."*

Wanafunzi wawili wa mwanzo walioitwa na Yesu walikuwa Simoni Petro na Andrea. Hawa ndugu

wawili walikuwa nje pamoja wakizitupa nyavu zao katika bahari ya Galilaya wakijaribu kuvua samaki. Yesu aliwaita na kusema "*Nifuateni nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu."*

Kutoka pale, Yesu alikwenda mpaka akaja kwa mtu na wanae wawili ambao walikuwa wamekaa katika mtumbwi wao wa kuvulia samaki, wakizitengeneza nyavu zao. Yesu aliwaita wale wana wawili kumfuata yeye. Maji naowa likuwa Yakobo na Yohana na jina la baba yao aliitwa Zebadayo. Kisha Yesu alizunguka katika Galilaya yote. Akifundisha katika masinagogi ya Kiyahudi na kuhubiri Habari Njema ya ufalme na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna. Habari zake zikaenea kiasi kwamba hata watu kutoka nchi jirani za Siria wangekuja ili kuponywa na Yesu.

Hivyo baada ya kuona kwamba watu wote hawa walikuwa wakimfuata yeye, aliwachukua wanafunzi wake, na akapanda juu ya mlima. Kule aliketi chini na kuwafundisha wanafunzi wake mambo mengi kuhusu ufalme wa Mungu.

Wakati walisikiliza mafundisho ya Yesu walishangaa kwa mamlaka aliyokuwa nayo. Hakuna yeyote aliyewahi kumsikia yeyote kama huyu katika sinagogi lake mwenyewe.

Wakati Yesu aliposhuka kutoka mlimani, makutano walikuwa tayari wakimsubiri kumfuata yeye popote atakapokwenda. Mtu mmoja mwenye ukoma alikuwa miongoni mwa makutano na akamuomba Yesu ikiwa angetaka kwa hiari yake kumtakasa juu ya ugonjwa

wake. Mara moja yule mtu akapona. Mtu mwingine, askari wa Kirumi, alimuomba ikiwa angemponya mtumishi wake kiwete aliyekuwa amelala nyumbani. Yesu alimponya yule mtumishi.

Yesu alikwenda kwa nyumba ya Simoni Petro kwa sababu mama mkwe wa Petro alikuwa anaugua homa na alikuwa mgojwa sana hajiwezi. Yesu alimgusa mkono na homa ikamwacha. Naye kisha akaamka na akawatumikia kila mmoja katika nyumba ile.

Hivyo yesu alikaa pale hadi jioni akiwaponya watu wote na akawatoa mapepo mengi. Lakini Yesu alipoona makutano mengi wakimzunguka mahali pale, Yesu aliamru wanafunzi wake kuondoka na yeye hadi ng'ambo ile ya Bahari Galilaya.

Ilikuwa tayari usiku wa manane wakati wote walipokuwa wamo katika mtumbwi na wakaanza safari kuelekea upande wa ng'ambo ya bahari. Ndipo ghafla, wakati walipokuwa wangali katikati ya bahari, dhoruba ikaja na ikaufunika mtumbwi kwa mawimbi. Wanafunzi wengi , wakiwa ni wavuvi, walitambua hatari waliyokuwa nayo na wakajawa na woga. Yesu, kwa vyovyote alikuwa amelala usingizi na hakuamka.

Wale wanafunzi wakiwa wamebaha, walimuamsha Yesu wakisema, **"*Bwana tuokoe! Sisi tunaangamia.*"** Yesu akawaambia wanafunzi, ***"Mbona mmekuwa waoga, enyi mlio na imani haba?"*** mara akaamka akazikemea pepo na bahari kukawa shwari kuu. Wale wanafunzi wakamaka, wakisema, huyu ni mtu wa namna gani hata pepo za bahari zinamtii?

MASWALI YA MDOMO

1. Yesu alihubiri ujumbe gani kwa watu?

2. Ni nini iliyokuwa kazi ya wanafunzi wa Yesu wa kwanza?

3. Ni kwa nini watu, kwa hali yoyote, walitaka kumuona Yesu?

4. Baada ya Yesu kushuka chini toka mlimani, alimponya mtu aliyekuwa na shidakubwa ki-afya. Ni nini iliyokuwa shida ya huyu mtu?

5. Yesu kisha alimponya mtumishi wa askari wa Kirumi. Lilikuwa tatizo gani kwa mtumishi huyu?

6. Yesu alimtibu mmoja wa jamaa ya Petro. Ni jamaa yupi?

7. Ni kwa nini Yesu alitaka kuvuka kwenda upande mwingine wa Bahari ya Galilaya?

8. Yesu alifanya nini juu ya mtumbwi?

9. Ni kwa nini wanafunzi wa Yesu walishikwa na woga?

10. Ni kwa nini Yesu aliwakaripia wanafunzi wake?

11. Wanafunzi waliuonaje uwezo wa Yesu wa kutuliza dhoruba?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 4-8

SOMO LA 4

1. **Yesu anatuita sisi sote kuwa "wavuvi wa watu."** Uhuru tulio nao katika Kristo ni kitu Yesu anatuamuru sisi kushirikisha watu katika kila nchi, mji na ujirani wa ulimwengu. Haya ndiyo yaliyokuwa maneno yake ya mwisho kwa wafuasi wakekabla yake kurudi mbinguni. Kwenye juma la mwisho la somo hili tutakwenda kujifunza jinsi gani ya kushirikisha imani yetu katika Yesu waziwazi. Kwa vyovyote, wengi wetu wanaogopa hata kuanza kushirikisha Kristo pamoja na watu wengine. Sisi tunafikiria vitu kama vile, "mimi ni nani pamoja na vizuizi vyote. Jinsi gani mimi ninaweza hata kumshawishi mtu fulani kumpokea Kristo? Na hata kama ningeweza, ninaishi tu katika pengo moja dogo la dunia, jinsi gani Kristo anatarajia sisi kufanya mabadiliko katika sehemu zingine za dunia?"

   Biblia inatufundisha kwamba hata ikiwa sisi ni mastadi wa michezo ya kuigiza na wastadi wa kusema ambao hawajawahi kuishi, bado kamwe

tusingeweza kumshawishi mtu kumfuata Kristo. Wakati sisi tulipotoa mioyo yetu kwa Kristo, haikuwa mtu aliyetugusa sisi, lakini uwepo wa Roho Mtakatifu wa Mungu aliyetuelekeza sisi kutubu. Yohana 16:8 inasema, “Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi na haki na hukumu.”

Wajibu wetu kama wavuvi wa watu ni kushikilia nje nguvu za maisha yetu na kuwaleta ndani samaki wote ambao Roho Mtakatifu anawaleta kwa njia yetu.

Moja ya hatua za mwanzo katika kushirikisha imani yetu katika Kristo pamoja na wengine ni kwa kuwa na uwezo wa kuwashirikisha yale Kristo aliyokwisha fanya katika maisha yetu. Hii aina ya mawasilisho inaitwa “Ushuhuda.” Neno “Ushuhuda” ni neno linalotumiwa katika mahakama za kisheria. Mashahidi hutoa ushahidi kwa mambo ambayo wanayaelewa kuwa ni ya kweli, mambo ambayo wao wameyashuhudia kwa mara ya kwanza.Ushuhudawa mtu ni njia ya binafsi na rahisi sana kwa kushiikisha Kristo kwa mtu fulani ambaye hajamjua Yesu. Hapa kuna mfano mzuri wa kufuata.

- Ebu kila mtu afikirie nyuma kwa jinsi gani maisha yake yalivyokuwa kabla hawajamjua Yesu.

- Kisha fikiria jinsi Kristo alivyojulishwa kwako kwa mara ya kwanza.

- Fikiria kuhusu wakati Roho Mtakatifu alihamia ndani ya moyo wako, na wewe ukajua ya kwamba Yesu alikuwa Mungu na ulimhitaji katika maisha yako.

- Fikiria juu ya uamuzi wako wa kutoa maisha yako kwa Kristo.

- Mwishoni, fikiria kuhusu tofauti Kristo aliyoifanya katika maisha yako.

- Baada ya kuwa na muda wa kuendeleza hii katika mawazo yako, ebu twende kwa mzunguko wa duara na ruhusu kila mtu kuanzia kiongozi ashirikishe ushuhuda huu pamoja na kikundi. Ni muhimu kwamba usichukue zaidi ya dakika tatu.

- *Kiongozi – Ikiwa kikundi chako ni kikubwa gawanya kikundi katika makundi madogo ya watatu au wanne ili kwamba kila mmoja apate zamu ya kushirikisha ushuhuda wake.*

- Pia ndio wakati, kama kikundi kuanza kumtegemea kila mtu kwa maombi wakati wa muda wetu wa kimya kwa ajili ya wale watu ambao Mungu ametuonyesha sisi kuwa wanahitaji kumpokea Kristo, labda wapo watu kutoka kazini au shuleni. Huenda pakawepo wana-familia wa karibu ambao bado hawajaupokea upendo wa Kristo. Omba

pamoja kwa ajili ya watu hawa. Ebu kila mtu aandike chini katika daftari yake majina yaliyotajwa na kila mmoja katika kikundi. Hiki ni juhudi za kikundi kwa kuleta kila mmoja kwa Kristo.

2. **Yesu aliwakaripia wanafunzi, sio kwa sababu walimuamsha kutuliza dhoruba, lakini kwa sababu wanafunzi walikuwa wamejawa na woga.** Wanafunzi waliangalia huku na huko ile dhoroba. Walikuwa na mazoezi ya dhoruba hii ni ile mbaya. Kitu ambacho hawakuwa nacho ni mazoezi ya uwezo wa Mungu katika maisha yao. Wanafunzi walikuwa bado kutambua kuwa Mungu ni mkuu kuliko dhoruba ya aina yoyote, na Yesu alikuwa amekaa nao katika mtumbwi.

naye mwanangu msichana wa mwaka mmoja na nusu ambaye ameanza kuvumbua ulimwengu unaomzunguka. Msichana huyu huwa anakimbia kuzunguka nyumba. Anafungua saraka, anatoa vyungu na vikaango na kila chochote anachoweza kupata katika mikono yake midogo. Siku moja tulikuwa kwa nyumba ya rafiki yangu tunakula chakula cha usiku. Msichana wangu alikuwa anacheza kwenye sakafu katika chumba chao cha maakuli, wakati huo sisi tunaendelea kula mpaka mbwa wao mkubwa mweusi akaja akitembea pole pole ndani ya chumba. Mwanangu mara moja akakimbia upesi jinsi miguu yake midogo ilivyoweza kumbeba akipaaza sauti. “Mama!” Nilimnyanyua na mara moja misuli yake ikalegea katika mikono yangu. Kwa nini? Kwa sababu alielewa kwamba mimi ninampenda yeye na

alinitumaini mimi kumtunza ilikuwa lakini dakika chache mpaka alipokuwa kabisa ametulia na hata alivyonyosha mkono wake kumbembeleza yule mbwa.

Sisi ni watoto wa Mungu tangu wakati tunapompa Yesu utawala wa maisha yetu. Yeye ni mlinzi wetu. Yeye ndiye usalama wetu na usalama kwa ajili ya watoto wetu. Yeye anatupenda sisi na katika woga wetu tunapaswa mara moja kukimbia kwake. Katika mikono yake anaondoa woga. Hakuna woga wakati tunaishi maisha yetu ya kila siku chini ya mabawa ya utiifu kwa Yesu kristo.

Kulikuwa na mtu mmoja katika Agano la Kale aliyeitwa Daudi. Yeye alipitia shida nyingi na mara nyingi kupungukiwa kwa sababu mtu aliyeitwa mfalme Sauli alijaribu kumuua. Jinsi Daudi alivyojifunza kweli nyingi kuhusu Mungu na akakua karibu na Mungu, aliandika utenzi mwingi unaoitwa “Zaburi.” Hizi ni tenzi zilizovuviwa na Mungu kwa kufundisha kuhusu Mungu. Zipo tenzi 150 ya hizi, sio za Daudi, lakini zote zinapatikana katika Agano la kale. Daudi aliandika Zaburi kadhaa kuhusu woga, lakini mimi nimechagua moja kwa ajili yetu kwa kusoma na kutafakari wakati wa juma hili – Zaburi 27. uisome wakati wako wa maombi juma hili. Ikiwa wewe hauna Agano la kale, mimi nimenakili kwa ajili yako Zaburi hii na kuijumuisha katika kitabu hiki. Muombe Mungu ili akufundishe wewe kuweka chini woga wote na

kupanda juu ndani ya mikono yake ya upendo na usalama.

- Maliza juma hili katika maombi, lakini safari hii ebu kila mshiriki ampate mwenzi hasa itakuwa bora wa jinsi ile ile. Zungumza kwa kila mtu na mwenzake kuhusu mambo katika maisha yako unayoogopa sana. Kisha omba kwa kila mmoja na mwenzake kuhusu woga, yataje bayana mbele za Bwana. Muombe Mungu kutupilia mbali woga na kuweka mbadala wa imani katika yeye. Mwambie Mungu juu ya shauku yako ya kuweka matumaini yako yote katika yeye, hata kuhusu vile vitu ambavyo vinaogopesha.

ZABURI 27:

Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu.
Nimwogope nani?
Bwana ni ngome ya uzima wangu.
Nimhofu nani?

Watenda mabaya waliponikaribia.
Wanile nyama yangu
Watesi wangu na adui zangu,
Walijikwaa wakaanguka.
Jeshi lijapojipanga nami,
Moyo wangu hautaogopa.
Vita vijaponitokea,
Hata hapo nitatumaini.
Neno mojanimelitaka kwa Bwana,
Nalo ndilo nitakalolitafuta.
Nikae nyumbani mwa Bwana,

Siku zote za maisha yangu.
Niutazame uzuri wa Bwana. Nakutafakari hekaruni mwake.
Mradi atanisitiri bandani mwake siku ya mabaya.
Atanistiri katika sitara ya hema yake
Na kuniinua juu ya mwamba.

Na sasa kichwa changu kitainuka
Juu ya adui zangu wanaonizunguka
Nami nitatoa dhabihu za shangwe hemani mwake,
Nitaimba, naam, nitamhimidi Bwana
Ee, Bwana, usikie, kwa sauti yangu ninalia,
Unifadhili, unijibu
Uliposema, nitafuteni uso wangu,
Moyo wangu umekuambia
Bwana uso wako nitautafuta.
Usinifiche uso wako,
Usijiepushe na mtumishi wako kwa hasira.
Umekuwa msaada wangu, usitupe
Wala usiniache, Ee Mungu wa wokovu wangu
Baba yangu na mama yangu wameniacha
Bali Bwana atanikaribisha kwake.

Ee Bwana unifundishe njia yako
Na kuniongoza katika njia iliyonyooka;
Kwa sababu yao wanaoniotea;
Usinitie katika nia ya watesi wangu;
Maana mashahidi wa uongo wameniondokea,
Nao watoao jeuri kama pumzi.
Naamini ya kua nitauona wema wa Bwana katika nchi ya walio hai.
Umngonje Bwana, uwe hodari,

Upige moyo konde, naam umngonje Bwana!

UPENDO – MAANA YA HUDUMA YA YESU DUNIANI

MATHAYO 8-10

SOMO LA 5

"Na alipowaona makutano, aliwahurumia kwa sababu walikuwa wamechoka na kutawanyika kama kondoo wasio na mchungaji." Mathayo 9:36

- Kabla ya kuanza somo hili, tafadhali chunguza ili kuona ni watu wangapi wamekuwa na nafasi ya kuwa na muda pekee pamoja na Kristo. Ni muhimu usiwe wa kuwasuta, lakini katika upendo, uwatie moyo wa kila mmoja na mwingine ili kukaa katika Neno la Mungu kila siku. Mualike kila mtu ili kuendelea kusoma kitabu cha Mathayo mpaka mwisho kabisa. Uliza ikiwa washiriki wamekuwa wakiomba kwa ajili ya watu ambao walikuwa wametajwa kwamba wanamhitaji Kristo. Ona ikiwa yeyote alipata wasaa wa kushirikisha ushuhuda wake wakati wa juma.

MARUDIO:

1. Nabii Isaya alisema kwamba Yesu angeitwa Imanueli, ikiwa ina maana ya "Mungu _____ _____."

2. Yesu alisema kwamba wakati yeye atakaporudi mara ya mwisho duniani _____ watamwona yeye akija katika mawingu na uwezo mkuu na utukufu.

3. Yesu alisema kwamba hakuna hata mmoja ajuaye ni lini yeye atarudi duniani ila _____.

4. Yohana aliwabatiza wengi huko nyikani ambao walitubu dhambi _____ zao.

5. Yohana alisema yuaja mmoja ambaye angewagawa watu wa ulimwengu na wale ambao walimkataa, wangehukumiwa kwa _____ usiozimika.

6. Yesu alimjibu Shetani safari tatu akitumia _____ la Mungu.

7. Ikiwa sisi tunataka kuwa karibu na Mungu, lazima tutumie muda wetu pekee pamoja na yeye _____.

8. Yesu alituita sisi sote kuwa _____ wa watu.

9. Wakati wa dhorubaalikuwa anafanya nini juu ya mtumbwi?

10. Ni kwa nini wanafunzi wa Yesu walishikwa na woga?

11. Yesu aliwakemea wanafunzi wake kwa sababu walikuwa _____ na wao hawakumtumaini yeye.

12. Biblia inatufundisha sisi kwamba wakati tunaishi chini ya ulinzi wa mabawa ya Kristo hatuna haja ya kuwa _____.

Baada ya kuvuka bahari ya Galilaya wakati wa dhoruba ya kurisha, Yesu na wanafunzi wake walifika ng'ambo ya upande mwingine wa bahari na pale mahali walikutana na watu wawili wenye pepo. Watu hawa walikuwa wakilia na walikuwa wakiishi makaburini. Ghafula mmoja wao akalia kwa sauti Yesu, "Tuna nini nawe, Yesu, Ewe mwana wa Mungu? Je, umekuja kututesa kabla ya muhula wetu?"

Mbali kidogo kutoka mahali ambapo wale watu wenye pepo walikuwako na kundi la wachungaji wakiangalia kundi la nguruwe wakilisha karibu na mwambao. Pepo walimuomba Yesu kwamba iwapo alikuwa anaenda kuwafukuza kutoka kwa miili ya wanadamu, awaache waende waingie miili ya nguruwe. Yesu akakubali akasema "Nendeni"! Wakati pepo walipoingia katika nguruwe wote waliruka kwa nguvu na hawakuweza kuthibitiwa,

wakateremka kwa kasi gengeni hata baharini, na wakafa majini.

Wale wachungaji wakakimbia katika ea kwa nguruwe. Watu wa mjini mji wakimwambia kila mmoja kile kilichotokea kwa wale watu sambamba na kile kilichotokea wakatoka nje na kumsihi Yesu kuondoka mkoani mwao. Yesu alipanda katika mtumbwi wake na kurudi Galilaya.

Baada ya kurudi Galilaya, mtu aliyepooza akaletwa kwa Yesu alimtibu yule mtu kule kupooza kwake na vile vile wakamtukuza Mungu, lakini Mafarisayo wakamwona kuwa Yesu anakufuru.

Akiendelea mbele kutoka pale, Yesu akamfikia mtoza ushuru jina lake Mathayo. Yesu alimwita Mathayo kumfuata na mara moja Mathayo akafanya hivyo. Yesu alikwenda kula na Mathayo sambamba na watoza ushuru wengine na watu wenye sifa za kutisha katika mji. Wakati Mafarisayo walipoona ni akina nani Yesu aliyekuwa anakula nao, waliwauliza wanafunzi wa Yesu ni kwa nini Yesu amefanya hivi. Yesu aliwajibu Mafarisayo akisema, “Nataka rehema na sio sadaka.”

Basi Yesu alitoka mahali pale na akawaendea watu wote kutoka kila aina ya maisha. Palikuwa na mtu mwingine aliyekuwa mtawala miongoni mwa watu wake. Huyu mtu alikuwa na mwanae wa kike ambaye alikuwa amefariki. Yesu alikwenda

kwenye sherehe za maombolezo akamshika mkono yule msichana na akamuinua kutoka wafu.

Yesu aliwarudishia uwezo wa kuona vipofu wawili waliomfuata na wakamuomba awapoye. Yesu alimrudishia uwezo wa kusema mtu ambaye hakuwa tu bubu bali alikuwa mwenye pepo. Aliwatoa pepo na yule mtu akapona.

Yesu aliyaona mahitaji mengi ya watu na akashikwa na huruma. Mahitaji yalikuwa makubwa mno, watu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, “Mavuno ni mengi lakini watenda kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno, apeleke watenda kazi katika mavuno yake.”

Yesu kisha akachukua wanafunzi wake na kuwatuma nchini kote katika Israeli. Yesu aliwapa uwezo wa kukidhi mahitaji mengi ya watu; kusudi lao ilikuwa kushirikisha na kuonyesha upendo wa Yesu. Yesu aliwapa maagizo maalum ya kutafuta watu ambao wako tayari kusikiliza Habari Njema ya Kristo. Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba wakati watakapowapata watu wa namna hiyo, wangeliacha amani ya Mungu juu ya miji yao. Lakini Yesu alionya kwamba wengi watawakatalia na maneno yao.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake, “Mimi nawatuma kama kondoo kati ya mubwamwitu. Basi iweni na busara kama nyoka, na kuwa watu wapole kama hua.” Aliwaambia wanafunzi

wakewasihangaike kuhusu mahitaji ya kimwili. Kwa kuwa Baba ambaye anajua hata idadi ya nywele juu ya kichwa chako yeye ndiye mtawala wa vitu vyote na anatuthamini sisi mno.

Yesu alikamilisha maneno yake kabla ya kuwatuma akisema, “Na mtu yeyote atakayemnywesha mmojawapo wa wadogo hawa ingawa kikombe cha maji baridi, kwa kuwa ni mwanafunzi, amini nawaambia haitampotea kamwe thawabu yake.”

MASWALI YA MDOMO

1. Watu wale walikuwa wakoje waliokutana na Yesu upande ule mwingine wa bahari baada ya safari ya kutisha ya mtumbwi?

2. Yesu alifanya nini kwa watu hawa?

3. Ni kwa nini nguruwe walijitupa wenyewe katika bahari?

4. Ni kwa nini watu wa mjini walimsihi Yesu kuondoka mkoani mwao?

5. Ni kitu gani Yesu alichofanya kwa ajili ya mtu aliyepooza?

6. Ni kwa nini Mafarisayo walimwita Yesu kuwa anakufuru?

7. Ni kwa nini Mafarisayo walimsuta Yesu na washirika wake wa chakula wakati Yesu alipokwenda kula pamoja na Mathayo na marafiki zake?

8. Ni nini lililokuwa jibu la Yesu kwa Mafarisayo?

9. Yesu alifanya nini kwa ajili ya mtoto msichana mwana wa mtawala?

10. Yesu alifanya nini kwa ajili ya vipofu?

11. Jinsi gani Yesu alivyomponya mtu ambaye hakuweza kusema? Alikuwa na shida gani?

12. Yesu aliwatuma wanafunzi wake kwenda kufanya nini?

13. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuweni na busara kama _____ na wasio na madhara kama _____.

14. Yesu aliwaambia wanafunzi wake wasiwe na wasiwasi kwa mambo ya aina gani?

15. Yesu alisema kwamba Mungu anajua idadi ya _____ ambazo tunazo.

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 8-10

SOMO LA 5

1. **Yesu anamjali kila mtu.** Yesu anawajali wenye pepo, wagonjwa, maskini, matajiri na hasa watoto. Kila mmoja ana thamani na anastahili katika ufalme wa Mungu!!!

2. **Wanadamu siku zote hawawajali watu wengine.** Katika kukabiliana na watu wenye pepo; watu wa mjini walikuwa wanahangaikia nguruwe kiasi kwamba wao walitaka Yesu aondoke katika mkoa wao. Wale watu wa mjini hawakujua lolote kuhusu yale yote Yesu aliyoyatenda kuwasaidia wale watu. Hawa watu wa mjini walihusika hasa kuhusu hasara zao za kifedha. Ni jambo rahisi sana kuthamini fedha kuliko watu. Kwa bahati mbaya, wengi wetu tunaanguka katika mtego huu. Tomotheo wa kwanza 6:10 inasema, "*Maana shida moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha: ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na imani na kujichoma kwa maumivu mengi, "Wewe, pia unaweza kukumbuka maneno ya Yesu katika Mathayo 6:19-21* mahali Yesu anasema, *"Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo na wezi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusiko haribika kitu kwa nondo wala kutu wala wezi hawavunji wala kuiba. Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako."*

- Fikiria; jinsi gani mimi ninavyotumia pesa zangu kila juma?

- Uliza swali, je, mimi ninamheshimu Yesu kwa jinsi gani ninavyotumia pesa zangu?

- Je, nimo ninanunua vitu au kufanya mambo ambayo yatavunja heshima kwa Mungu? Je, mimi nimo ninaumiza wengine kwa namna ninavyotumia pesa? Je, mimi nimo ninawasaidia wengine kwa namna ninavyotumia pesa zangu?

Katika Agano la Kale, Mungu alitaka kila mtu kutoa asilimia kumi 10% ya yale aliyo nayo kwa Mungu. Katika Agano jipya. Tunaambiwa sisi kutoa maisha yetu na kila kitu tulicho nacho kwa Mungu. Kimapokeo, waumini wamefuata sheria ya Agano la Kale na kutoa 10% ya mapato yetu ya kifedha kwa kazi ya Mungu au kanisa. Hii inaitwa zaka. Anza kuomba sasa, ni kiasi gani cha pesa zako Bwana anazotaka wewe utoe kwa kazi yake? Biblia inatufundisha kwamba Mungu huwabariki wale ambao wanachangia kwa kukua kwa ufalme wake. Biblia pia inafundisha Yesu atatupa mahitaji yetu yote. Wewe unaweza ukawa unafikiria, “Lakini Mungu haelewi jinsi gani mimi nilivyo maskini? Mungu huwa haelewi jinsi gani ukubwa wa deni nililofanya mimi mwenyewe?” Yesu alizaliwa vilevile katika familia maskini sana ya kidunia. Yesu anaelewa matatizo ya umaskini, lakini Yesu anatutaka sisi sote kuwa waaminifu

katika kutii kwa lolote analotutaka sisi tufanye. Muombe Bwana, jinsi gani yeye anavyotaka wewe uwe sehemu ya kutegemeza kifedha huduma yake.

3. **Wewe unaweza kuonyesha upendo kwa Mungu na kwa wengine kwa kutoa zaka kwa kazi ya Mungu kupitia kwa kanisa lako.** Mungu anatumia makanisa kuhudumia matatizo ya watu kiroho, kimaono na kimwili Mungu anatumia zaka yako kuisaidia kanisa kutimiza majukumu yake.

- Ikiwa wewe sio mshiriki wa kanisa, muulize kiongozi wako jinsi gani wewe unavyoweza kujihusisha.

4. **Kuwa mfuasi wa Kristo ina maana kufuata mfano wake na kupenda wengine kama Yesu alivyofanya.** Ni kweli kwamba sisi hatuwezi kuwaponya watu kama Yesu alivyofanya , lakini **bado Yesu anatibu na kuponya watu.** Tunapashwa sisi kuwa waaminifu kuomba kwa ajili ya wagonjwa. Tunapashwa kuwepo kandokando upande mwao na kushika mikono yao wakati wanapokuwa na maumivu. Tunapashwa sisi kuwaambia wao juu ya upendo wa Yesu kwa ajili yao. Tunapashwa kuomba kwa ajili ya wenye pepo. **Yesu bado anatoa pepo** ulimwengu mzima kupitia kwa maombi ya watu wa Yesu. Sisi tunapaswa kuomba kwa ajili ya kusaidia mahitaji. Tunapashwa sisi kufanya chochote tunachoweza kusaidia kwa mahitaji yao ya kimwili na hususani

kuwaambia wao kuhusu upendo wa Kristo ambaye anaweza kubadili maisha yao ya ndani. Sisi tunapshwa hasa kusaidia watoto. Yesu aliwaamuru wanafunzi wake kufanya mambo hayo yote, lakini Yesu aliahidi thawabu maalumu kwa watu ambao watawasaidia watoto.

5. **Baadhi ya watu sio rahisi kuwapenda, lakini Mungu anashauku juu yetu kuwa na rehema.** Watoza ushuru wakati siku hizo walikuwa wanachukiwa kwa sababu moja nzuri. Waliifanyia kazi serikali dhalimu wakikusanya pesa kutoka kwa watu. Wengi wao waliwatoza watu zaidi kuliko zilizokuwa zinadaiwa na kuweka mfukoni mwao iwe ziada kwa manufaa yao. Kuonyesha upendo kwa mtu ambaye amekuibia kitu fulani kutoka kwao sio rahisi, hasa ikiwa mtu huyu sio wa kutubu hata kidogo kwa kile alichokifanya. Yesu anatuambia sisi kwamba kama wafuasi wake hatuna haki ya kuhukumu watu hawa ikiwa yale wanayoyafanya ni mabaya kabisa. Kazi yetu ni kuomba kwa ajili yao, kuwapenda wao, na kuwaonyesha wao ukweli kuhusu msamaha wake Mungu. Ikiwa watatubu juu ya dhambi zao, wao tena watapatiwa msamaha kamili wa Mungu. Biblia inasema sisi tumesha pokea rehema, hivyo tunapashwa sisi pia kuonyesha msamaha na rehema, hata ikiwa ni karibu kitu kisichowezekana kwetu sisi

kukifanya pasipo uweza wa Mungu katika maisha yetu.

MASWALI YA MAJADILIANO

1. Nikatika njia zipi ambazo mimi naweza, katika hali yangu ilivyo na katika ulimwengu wangu, kuonyesha upendo wa Mungu na rehema kwa wengine?

2. Ni nini mahitaji makubwa ya watu wanaonizunguka? Jinsi gani watu wanavyoumiza zaidi mahali mimi ninaishi?

3. Jinsi gani mimi ninavyoweza kuwafikia watu wanaoumia wanaonizunguka mimi?

4. Jinsi gani mimi naweza kuonyesha upendo wa Mungu hasa kwa watoto?

5. Ni katika njia gani mimi ninavyoruhusu pesa zije mbele ya watu katika maisha yangu?

6. Je, mimi namheshimu Mungu kwa pesa zangu?

7. Wewe unafikiriaje juu ya mchango wa pesa kwa kanisa?

KUSALITIWA NA MSAMAHA
MATHAYO 21-27:10

SOMO LA 6

"Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote'' 1 yohana 1:9.

MARUDIO

1. Nabii isaya alisema kwamba yesu angeitwa Imanueli, ikiwa na maana "Mungu

   _____ _____."

2. Yesu alisema kwamba hakuna hata mmoja ajuaye ni lini atarudi ulimwenguni Isipokuwa_____.

3. Yohana alibatiza wengi huko nyikani ambao walitubu juu ya _____zao.

4. Yesu alimjibu shetani safari tatu akitumia _____la mungu.

5. Ikiwa sisi tunataka kuwa karibu na mungu, lazima tutumie muda pekee pamoja na mungu

6. Yesu alituita sisi sote kuwa _____wa watu.

7. Yeyealionyesha upendo kwa watu wote kwa_____wao maradhi yao.

8. Yesu aliwaambia wafuasi wake kwenda nje kwa watu wote lakini wawe na busara kama _____ na kutokuwa na madhara kama hua.

9. Yesu anasema kwamba yeye anajua idadi ya _____zilizopo juu ya vichwa vyetu.

10. Yesu aliwaambia wanafunzi wake ndani ya mtumbwi wasiwasi na _____.

Yesu alifundisha, alihubiri na akawaponya watu wengi katika mkoa wa Galilaya, lakini bado wengi waliyakataa maneno yake. Yesu aliwaeleza wanafunzi wake kwamba hii ilikuwa vile ni kufuatana na mpango wa Mungu kwani alichagua kuficha ukweli wake wenye hekima na akili na kuwafunulia watoto wachanga.

Muda uliwadia ambao Yesu alikuwa amewaeleza mapema. Ilikuwa ni wakati wake wa kwenda Yerusalemu, kwa ajili ya kuteseka mambo mengi kutoka kwa wakuu wa makuhani na viongozi wengine wa dini, kuuwa na kuinuliwa kutoka katika wafu.

Kuwasili kwake ndani ya Yerusalemu ilikuwa ni swala kubwa. Watu walijipanga mistari pande zote, kando kando ya barabara wakizitupa chini

nguo zao na matawi ya miti wakitengeneza jamvi kwa ajili ya Yesu kutembelea juu yake. Wakati alipokuwa akipita kati yao akiwa amekaa juu ya punda walipaza sauti, “Hosana mwana wa Daudi, ndiye mbarikiwa yeye ajaye kwa jina la Bwana! Hosana juu mbinguni!”

Yesu alikaa siku kadhaa katika Yerusalemu akifundisha katika hekalu, akihubiri na kuwaponya watu wengi. Kwa hali yoyote, Yesu alikabiliana na vipingamizi vingi na migongano na Mafarisayo na Masadukayo.

Yuda Iskarioti, mmoja wa wanafunzi wake Yesu mwenyewe, aliwaendea wakuu wa makuhani na akaahidi kumsaliti Yesu kwao kwa ajili ya pesa. Wakuu wa makuhani walimpatia vipande vya fedha thelathini. Yuda akavichukua.

Ule usiku wa sherehe za Pasaka, sikukuu maarufu sana kupita zote za Kiyahudi za mwaka, Yesu aliketi na wanafunzi wake kwa chakula cha mwisho pamoja. Penye chakula hiki, Yesu alitwaa mkate ambao walikuwa wakiula, akaumega na kusema, “Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu.” Kisha akainua kikombe cha divai, akashukuru juu yake na kusema, “Nyweni nyote katika hiki. Hii ni damu yangu ya Agano Jipya, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi.”

Baada ya chakula cha mchana, wanafunzi wote walikwenda juu ya mlima wa Mizeituni. Hapa

Yesu aliwaonya wanafunzi kwamba wao wote wangefanya kujikwaa. Petro kwa ukaidi alishikilia kwamba yeye kamwe asingemsaliti Yesu, lakini angemkana Yesu safari tatu kabla ya jogoo kuwika asubuhi ile yenyewe.

Tokea hapo, Yesu aliwapeleka wanafunzi wake hadi Gethsemane. Alitumia muda wote uliobaki wa usiku akiomba. Yesu alikuwa na huzuni nyingi kiasi cha kufa kwa sababu ya yale yote ambayo yalikuwa yanaenda kutokea. Yesu aliwataka wanafunzi wake waombe pamoja na yeye, lakini wote walilala usingizi. Wanafunzi wake waliamka tu wakati wa kuwasili kwa Yuda katika bustani pamoja na makuhani na watu ambao walikuja kumchukua Yesu.

Yusa alikuja kwa Yesu na akambusu kama dalili ya kusalitiwa kwake. Wakuu wa makuhani wakamshika Yesu na wakamchukua kwa nyumba ya kayafa, ambaye alikwa ni kuhani mkuu kwa nyakati zile. Wale wanafunzi wakakimbia kutoka Gethsamane.

Wakati ule alipokuwa katika nyumba akihojiwa na Kayafa na viongozi wengine, Petro alikuwa nje katika ua. Wakati Petro akiwa ameketi; kijakazi alikuja kwa petro na kumwambia, “Wewe nawe ulikuwa pamoja na Yesu wa Galilaya.” Petro akakana. Kisha Petro akasogea kwenye lango na akasubiri mpaka msichana mwingine alipomuona na kumshitaki Petro kwa

kuwa alikuwa pamoja na yesu. Petro vile vile akakana, safari hii kwa kiapo. Baadaye kidogo watu wengine, wakamwendea Petro na wakamshitaki kwa kuwa alikuwa pamoja na Yesu. Safari hii alianza kulaani na kuapa akisema, “Simjui mtu huyu?!” Mara moja jogoo akawika na Petro akayakumbuka maneno ya Yesu penye Mlima wa Mizeituni. Petro akatoka nje akaenda zake na kulia kwa majonzi. Na ilipokuwa asubuhi, wakuu wa makuhani walimpeleka Yesu kwa Pilato ili akahukumiwe kifo. Yuda baada ya kuona kwamba Yesu amehukumiwa kifo alijuta na akajaribu kuwarudishia wakuu wa makuhani, “Mimi nalikosa niliposaliti damu isiyo na hatia.” Wakuu wa makuhani wakamjibu, “Bai haya yatupasa ni sisi? Yaangalie haya wewe mwenyewe!” Yuda kisha akavitupa vile vipande vya fedha juu ya sakafu ndani ya hekalu, akaondoka kutoka pale na akajinyonga mwenyewe.

MASWALI YA MDOMO

1. Mpango wa Mungu ni kuficha ukweli kutoka kwa wenye busara na akili na kuwafunulia akina nani?

2. Jinsi gani alivyotendewa Yesu wakati alipoingia mji wa Yerusalemu?

3. Ni kwa nini Yuda aliwaendea wakuu wa makuhani na ni kwa nini walimpatia Yuda vipande thelathini vya fedha.

4. Wakati wa chakula cha mchana cha Pasaka ya mwisho cha Yesu pamoja na wanafunzi wake, Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba ile divai na ule mkate vilikuwa maalum. Jinsi gani hivyo?

5. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba damu yake lazima imwagike. Ni kwa nini?

6. Penye mlima wa Mizeituni, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba wangefanywa kujikwaa. Petro alikana. Kisha Yesu akatoa tabiri maalum kuhusu Petro. Utabiri huo ulikuwa nini?

7. Ni kwa kitendo gani Yuda alikitumia kumsaliti Yesu?

8. Petro alikuwa wapi wakati viongozi wa dini walipokuwa wakihoji Yesu?

9. Wasichana wawili walimjia Petro kwa nyakati tofauti na wakamshitaki kwa vitu fulani. Ni nini?

10. Kwa safari ya tatu, watu kadhaa walikuja na kudai kwamba Petro alikuwa pamoja na Yesu. Jinsi gani Petro alivyojibu watu hawa?

11. Ni wakati gani Yuda alipojisikia kuwa anayo hatia kwa ajili ya kumsaliti Yesu?

12. Ni kwa nini Yuda alikwenda tena kwa wakuu wa makuhani?

13. Yuda alifanya nini wakati wakuu wa makuhani walipokataa kuzipokea tena pesa za usaliti?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 21-27:10

SOMO LA 6

1. Wakati wa chakula cha mwisho cha Yesu pamoja na wanafunzi wake, alianzisha mafundisho ya kupokezana ambayo yamekuwa yakifuatwa na wafuasi wa Kristo ulimwenguni mzima tangia wakati ule hadi leo hii. Sisi tunaita mapokeo haya Chakula cha Bwana. **Chakula cha Bwana** sio tukio la kimiujiza ambalo linaondoa dhambi au kufanya vitu fulani maalum katika miili yetu. Sio wasaa ambao mkate wa kawaida na maji ya matunda kwa kiini macho vinakuwa damu ya Yesu na mwili. **Ni wasaa kwa wafuasi wa Kristo kuja pamoja kupitia kula mkate na kunywa kwa divai kwa ukumbusho wa sadaka ya Yesu juu ya msalaba.** Ni wakati wa kukumbuka gharama Yesu aliyolipia kwa ajili ya

dhambi katika maisha yetu. Ni wakati wa shangwe na shukrani jinsi tunavyofurahia pamoja katika msamaha Yesu alionunua kwa ajili yetu sisi. 2Wakoritho 11:23-33 inatufundisha sisi kwamba ni tukio muhimu, sio kitu cha kufanya kijuu juu. Ni wakati wa kutafakari juu ya sadaka yake kwa ajili yetu sisi na kuyachunguza maisha yetu wenyewe katika mwanga wa yale ambayo ametufanyia sisi juu ya msalaba.

2. **Mungu anajua kushindwa kwetu hata kabla hatujafanya na bado yeye anatukubali sisi na anataka kututumia sisi katika ufalme wake.** Toka wakati ule Yesu kwanza anamwita Petro angemsaliti. Jinsi tunavyoendelea kusoma Biblia zetu tutajifunza sisi katika Matendo ya Mitume kwamba Mungu alimtumia Petro kuongoza maelfu ya watu kwa Kristo. Kwa kweli kuna vitabu viwili katika Biblia ambavyo viliandikwa na Petro. Katika Matendo ya Mitume, sura ya pili, mara baada ya Yesu kurudi mbinguni, tunamuona Petro akihubiri kwenye Ibada katika Yerusalemu mbele ya maelfu ya viongozi wa Kiyahudi, watu wale ambao Petro aliwaogopa usiku ule wa uhaini.

   Katika njia hiyo hiyo, kushindwa kwetu sio jambo la kumshangaza Mungu. Hata baada ya kumpokea Kristo, sisi tutakuwa na kushindwa katika maisha yetu. Tutetenda dhambi, tutamlaliti, tutafanya vitu vile vile tunavyochukia.

3. **Tufanye nini baada ya kushindwa mbele zake Mungu?** Kulikuwa na watu wawili waliomsaliti

usiku ule. Mtu mmoja alikuwa Petro, lakini hatimaye alitumiwa sana na Mungu. Mwingine alikuwa Yuda ambaye naye pia alimsaliti Mungu, lakini kisha akajinyonga. Watu wengi kimakosa wanaamini kwamba sababu iliyomfanya Petro kufanikiwa na Yuda kushindwa ilikuwa kwa sababu kusaliti kwa Yuda kulikuwa kukubwa zaidi. Hii sio hivyo. Biblia inatufundisha kwamba sisi sote tu watenda dhambi. Sisi sote tulimsaliti Mungu na tunastahili adhabu ya milelekwa ajili ya usaliti wetu. Lakini ikiwa hii sio kweli, ni nini lililokuwa kosa la kuhuzunisha sana la Yuda? Yuda hakutubu dhambi zake na kutafuta msamaha wa Mungu.

Wapo watu wengi wanaojua wakati gani wamefanya mambo mabaya. Watu wengi hujisikia kuwa na hatia ya kutisha kwa mambo ambayo wameyafanya katika maisha yao kwamba yalikuwa mabaya. Baadhi ya watu wamefanya mambo ya kuhuzunisha ambao wao wanajisikia kwamba hata Mungu kamwe hawezi kuwasamahe wao kwa mambo haya. Biblia inatufundisha kwamba hii siyo kweli.

Yohana wa Kwanza 1:9 inasema, "*Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote."*

Hii ina maana kwamba ikiwa mtu:

- Anakuja mbele za Mungu

- Anamuambia Mungu ni nini alichokifanya

- Anatubu

- Anamuomba Mungu kumsamehe juu ya dhambi hii
- **Ndipo Mungu yu mwaminifu kumsamehe huyu mtu juu ya kitu chochote, haidhuru ni jinsi gani dhambi iliyo ya kutisha, sadaka Yesu juu ya msalaba inastahili tosha kuosha dhambi hii.**

Hii pia ina maana, kwamba kama mfuasi wa Kristo, tunapashwa kamwe tusiishi maisha ya kushindwa tukikumbuka dhambi zilizopita ambazo tayari zimeisha samehewa na Mungu. Sisi hatuhitaji kuishi katika hatia kwa mambo ambayo Kristo tayari aliisha yasahau. Petro alitubu juu ya dhambi zake na aliweza kutumiwa na Mungu.

Yuda kwa kweli alikuwa na uovu katika moyo wake. Ilikuwa ni jambo la kuudhi kwa kumsaliti rafiki wa karibu na kusababisha huyu mtu kuteseka na kufa kifo cha kutisha wakati Yesu alikuwa kabisa hana hatia ya kutenda mabaya. Kwa hali yoyote ukweli ni kwamba Mungu bado alikuwa na mpango kwa ajili ya maisha ya Yuda. Hata Yuda alikuwa anastahili msamaha wa Mungu. Sadaka ya Yesu ya uhai wake juu ya msalaba ilikuwa kubwa yakutosha kumsamehe hata Yuda. Ikiwa tungelikuja kwa Kristo, lakini badala yake aliruhusu hatia kutawala maisha yake. Ilikuja ikiwa zaidi ya kawaida na akayamaliza maisha yake mwenyewe.

4. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba **agano letu au makubaliano yetu na Mungu inafanyika kuwezekana kwa sababu ya damu ya Yesu ambayo ilimwagika kwa ajili ya msamaha wa dhambi** – siyo kwa sababu ya kitu chochote ambacho sisi tumekifanya. Sisi hatukufanya chochote kupokea msamaha wa Mungu katika maisha yetu. Mara tunapompokea Yesu ndani ya mioyo yetu, hakuna chochote tunachoweza kufanya kupoteza huu msamaha.

   Waefeso 1:13b-14 inasema, "Tena mmekwisha kumwamini yeye na kutiwa mhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu, ndiye aliye arabuni ya urithi wetu ili kuleta ukombozi wa milki yake, kwa sifa na utukufu wake." Yohana 3:16 inasema kwamba wewe unao "Uzima wa milele." Mara Kristo anapoingia kwako kwamwe hakuachi. Wewe umeokolewa daima tangu hatua hiyo na kuendelea. Biblia inasema kwamba tunapashwa kukumbuka sadaka ya Yesu kwa ajili yetu na kuacha kutenda dhambi. Sisi lazima tujitahidi kuishi kila siku maisha yaliyo na utiifu kamili kwa Yesu.

   Lakini katika waraka wa Kwanza wa Yohana 2:1 inatukumbusha sisi kwamba ikiwa tunatenda dhambi, lazima sisi tukumbuke ni nani anayeishi ndani yetu na ni kwamba ikiwa tunatenda dhambi, lazima sisi tukumbuke ni nani anayeishi ndani yetu na kwamba uwepo wake hautegemei juu ya matendo yetu. Lazima sisi tukumbuke kwamba Yesu yumo ndani ya maisha yetu kama mtetezi wetu mbele ya Baba. Yeye

hatatuacha sisi bila kujali yale tunayoyafanya. Yeye daima ni malipo badala kwa ajili ya dhambi zetu.

MAJADILIANO

1. Wewe unafikiria nini kuhusu Petro na kuhusu Yuda?

2. Neno “msalaba” lina maana gana kwako wewe?

3. Wewe uliisha wahi kujisikia una hatia ya jambo lolote unaloweza kujilinganisha na Yuda?

4. **Usisime chochote kwa sauti,** lakini Je, inawezekana kwamba ulifanya kitu fulani cha kushangaza ambacho wewe unaona vigumu kupokea msamaha wa Kristo katika maisha yako?

5. Ni yapi maneno ya Yesu kwako katika hali ya namna hii? **Hakikisha kila mmoja anasema mbele ya watu au unasoma kwa sauti Waraka wa kwanza wa Yohana 1:9** (imewekwa mwanzoni kabisa mwa somo hili.)

Kila mtu sharti ainamishe kichwa chake na aseme na Mungu yale yote ambayo yamo moyoni mwake. Ikiwa kunayo dhambi pale uiungame. Muombe Mungu kukutoa hatiani. Muombe Mungu, kwa rehema zake,

kukuweka mbali, kwa gharama yoyote, kutoka dhambi hii. Ungama waziwazi kwamba sadaka ya Yesu juu ya msalaba inatosha kukusamehe wewe dhambi zako. Dai ukweli huu kwa sababu imo ndani ya Neno la Mungu, hata ikiwa wewe haujisikii kwamba hii inawezekana.

- **Inawezekana kwamba baadaye, Shetani anaweza akajaribu kukushambulia kwa kukushitaki na mawazo ya hatia. Kwa mfano Shetani anaweza kusema, "Mungu kwa kweli hakukusamehe wewe, hii yote ni uongo. Hakuna mtu ajuaye jinsi gani wewe kwa kweli ulivyo." Mawazo ya namna hii huwa hayatokani na Mungu. Mawazo haya siyo hatia halisi, lakini hatia ya uongozi. Kuhusu kitu furani ambacho Mungu tayari ameisha kusamehe, mara moja acha kuwazia na omba. Sema:**

  "Ahsante Yesu kwa wokovu wangu na msamaha wako wa dhambi zangu (Taja dhambi yenyewe dhahiri.) ninaomba katika jina la Yesu kwamba uniondolee haya mawazo ya hatia katika akili zangu."

  Mungu ni mwaminifu, atafanya hili. Ikiwa utamuomba Mungu kila wakati Shetani anapokushambulia wewe, haitachukua muda kabla hajaacha kukushambulia katika maeneo haya, nawe utakuwa huru kwa mawazo haya ya hatia daima. Sisi tunao ushindi kamili juu ya kila eneo la maisha yetu katika Kristo.

KUSULUBIWA KWA KRISTO
MATHAYO 26-27

SOMO LA 7

“Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi bali kwetu sisi tunaokolewa ni nguvu ya Mungu.” 1Wakorintho 1:18

MARUDIO

1. Nabii Isaya alisema kwamba Yesu angeitwa Imanueli, ikiwa na maana ya “Mungu _____ _____.”

2. Yesu alisema hakuna yoyote ajuaye ni wakati gani Yesu atarudi ulimwenguni ila ni _____.

3. Yohana aliwabatiza wengi huko nyikani ambao walitubu juu ya _____ zao.

4. Yesu alimjibu Shetani safari tatu kwa kutumia _____ la Mungu.

5. Ikiwa sisi tunataka kukua karibu na Mungu na kuweza kupinga majaribu, lazima sisi tutumie muda wa _____ pamoja na yeye _____ _____.

6. Yesu aliwaita wanafunzi wake kuwa _____ wa _____.

7. Juu ya mtumbwi wakati wa dhoruba, Yesu aliwaambia wanafunzi wake wasiwe na _____ kwa sababu ya uwepo wake pamoja nao.

8. Yesu alitumia muda wake katika masinagogi aki _____ kuhusu ufalme wa Mungu na _____ magonjwa ya watu.

9. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwenda nje kwa watu wote, lakini wawe na _____ kama nyoka na wasiwe na madhara kama _____.

10. Yesu alisema kwamba yeye anajua hata idadi ya _____ juu ya _____.

11. Juu ya mlima wa Mizeituni Yesu alitabiri kwamba _____ angemsaliti safari tatu kabla ya Jogoo kuwika asubuhi.

12. _____ alikuwa ni mwanafunzi aliyemsaliti Yesu kwa ajili ya vipande thelathini vya fedha.

13. _____ alitubu juu ya usaliti wake na baadaye alitumiwa sana na Mungu.

14. _____ alijisikia kuwa na hatia mno kwa kile alichokitenda na akaondoka akaenda kujiua mwenyewe.

15. Biblia inatufundisha kwamba ikiwa sisi _____ dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki _____ dhambi zetu na kutusafisha kutoka _____ wote.

Wakati Petro alikuwa nje ya mlango kwa nyumba ya Kayafa, Yesu alikuwa ndani akiwa anashitakiwa kwa aina zote za ushahidi wa uongo. Hakuna hata moja iliyokuwa ya kusadikika vya kutosha kumtia hatiani. Yesu aliwaruhusu washiakiwa wake kuendelea kumshambulia bila hata ya kufumbua mdomo wake katika utetesi wake mwenyewe. Baada ya kushindwa kufanikisha lolote, Kayafa alimuuliza yesu,utuambie sisi kama wewe ndiwe Kristo,mwana wa Mungu!
Hatimaye yesu akavunja kinywa chake akasema, “wewe unasema ,lakini nawaambieni tangu sasa mtamwona Mwana wa adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu akija juu ya mawingu ya mbinguni.”

Hatimaye yesu akavunja kinywa chake akasema, “wewe unasema ,lakini nawaambieni tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu akija juu ya mawingu ya mbinguni.”

Huu ulikuwa ushahindi wa kutosha kwa kutosha kwa kayafa na akazirarua ngua zake na kusema kuwa Yesu amekufuru.Wakamchukua Yesu, wakamtemea mate usoni,wakamfanyia mzaha na kumpiga makonde wengine wakampiga makofi.

Na alipokuwa asubuhi,wakuu wa makuhani na viongozi wakamfunga wakampeleka kwa pilato,Liwali wa kirumi wa mkoa wa yuda. Liwali akamuulizia Yesu , “wewe ndie mfalme wa Wayahudi?”Jibu la Yesu lilikuwa rahisi. “wewe wasema .”Wakuu wa makuhani kisha wakazidi wakaendelea kuleta orodha yao ya mashitaka.Lakini yesu tena hata hakujibu .Hata liwali akastaajabu kwa ustadi wa yesu kwa kukaa kimya. Liwali hakumpata na hatia yeyote na akajaribu kupata njia ya amani ya kumuachilia.

Ilipokuwa pasaka.sikukuu Muhimu ya mwaka wa kiyahudi,imekuwa kila mara ni desturi ya pilato kumuachilia mfungwa mmoja kwa hiari ya watu.Mwaka huu pilato aliwaleta wawili mbele za wote.Mmoja alikuwa Baraba, mhalifu aliyechukiwa,na Yesu .pilato aliwauliza watu ni yupi kati ya hawa mnayemtaka ni waachilie. Wakiwa wavurugwa na wakuu wa makuhani, wakapiga kelele wakisema baraba aachiliwe na Yesu asulubiwe.Kisheapilato akapaza sauti kwa watu “kwa nini, ni ubaya gani

alioutenda?”Jibu lako lilikuwa “Mwache asulubiwe!”basi pilato alipoona ya kuwa hafahi loote,bali ghasia inazidi tu,hivyo mwenye haki.Yaangalieni haya ninyi

wenyewe.”Watu wakijibu kwa kusema, “Damu yake na iwe juu ya watoto wetu.”pilato akawafungulia Baraba na kuamuru Yesu kupingwa mijeredi na

kisha akatumwa kwa makao yake makuu yanayoitwa praitorio mahali angeendelea kuteswa.

Pale proitorio,walimvua nguo.wakamvika vazi jekundu.Wakampa mwanzi kuushika na kuiweka taji la miiba juu ya kichwa chake.Maasikari wakamdhihaki kumtemea mate.Wakapiga magoti mbele yake wakamfanyia mzaha mkubwa wa kwamba kweli Yesu alidai kuwa mfalme. Kisha wakauchukua mwanzi ambao umekuwa katika mikono yake wakampiga piga kichwani nao.

Baada ya askari kumaliza yote waliokuwa wanatarajia kufanya katika Praitorio, walimvua nguo wakamvika mavazi yake na wakamchukua hadi Goligotha, yaani “Fuvu la Kichwa.” Hapa palikuwa ni mahali ambapo usulubishaji ungefanyika. Wakati wangali kutoka Praitorio, walimlazimisha mtu mmoja jina lake Simoni kuubeba msalaba wa Yesu kwa ajili yake.

Wakati Yesu alikuwa akining’inia juu ya msalaba ma-askari waligawanya nguo za Yesu na wakapiga kura ili kuona ni nani angepata nini? Walimuangalia alipokuwa anakufa toka chini ya msalaba. Wakuu wa makuhani na wazee wengine pia walitoka kuja kuona Yesu hangeweza kushuka kutoka msalabani. Watu wengine wengi walikuja mahali pale aliposulubishwa wakitikisa vichwa vyao. Hata wale majizi wawili waliokuwa wamesulubiwa kwa kila upande wa Yesu hawakuweza kujizuia kufanya masimango ya chuki.

Basi tangia saa sita hadi saa tisa palikuwa na giza ilitanda ulimwengu mzima. Yesu alilia kwa Mungu “Eloi, Eloi lama sabakithani.” Ambayo ina maana, “Mungu wangu, Mungu mbona umeniacha?” Waliposikia kilio hiki, mtu fulani akaenda mbio, akatwaa sifongo akaijaza siki na akajaribu kumnywesha Yesu. Wale wengine wakasema, “Achana naye.” Ngoja tuone kama Eliya anakuja kumwokoa. Naye Yesu kishaakupaza sauti yake tena, akaitoa Roho yake.

Wakati wa kifo chake kulikuwepo maajabu mengi ambayo yalitokea Yerusalemu yote ikidhihirisha kuwa Yesu alikuwa nani. Pazia ya hekalu ilipasuka vipande viwili ambalo lilikuwa limetenga mahali patakatifu pa patakatifu; nchi ikatetemeka, miamba ikapasuka. Vile vile makaburi mengi yalifunuka na miili ya wafuasi wa Kristo ambao walikuwa waliisha fariki ikainuka kutoka makaburini na wakatembea wakizunguka mji wa Yerusalemu.

Jioni ya kifo cha Yesu, mtu tajiri sana jina lake ni Yusufu wa Arimathaya alikwenda kwa Pilato na akaomba ikiwa angeuchukua mwili kwenda kuuzika. Pilato alikubali na Yesu akapelekwa kwenye kaburi jipya kabisa ambalo lilikuwa limechongwa katika mwamba. Yusufu akauchukua mwili wa yesu, akautwaa mwili wa Yesu, akauzonga-zonga katika

sanda ya kitani safi, akamlaza Yesu chini katika pango na akaviringisha jiwe kubwa mbele ya mlango wa kaburi kabla ya kuondoka pamoja na Maria

Magdalena na Maria yule mwingine kutoka mahali pale.

MASWALI YA MDOMO

1. Jinsi gani viongozi wa Kiyahudi mwishoni walivyomtia hatiani Yesu katika hukumu iliyotolewa penye nyumba ya Kayafa.

2. Jinsi gani Yesu alivyojibu kwa mashitaki yote dhidi yake mbele ya Pilato?

3. Jinsi gani Pilato alimchukulia Yesu kwa stadi yake ya kubakia kimya mbele ya washitaki wake wote?

4. Baraba alikuwa nani?

5. Jinsi gani askari wa Kirumi walivyomtendea Yesu?

6. Jinsi gani makuhani na watazamaji wengine walivyomtendea Yesu wakati Yesu alipokuwa amening'inia juu ya msalaba?

7. Kulitokea nini ulimwenguni kote katikati ya saa sita na saa tisa?

8. Ni mambo gani ya ajabu yaliyotokea wakati wa kifo cha Yesu?

9. Yusufu wa Arimatha yaalifanya nini na mwili wa Yesu?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 26-27

SOMO LA 7

Njia za Mungu sio njia za mwanadamu. Ebu sisi tusome kwa pamoja fungu la maneno katika Maandiko Matakatifu yanayopatikana katika Wakorintho wa Kwanza 1:18-27. Somo kifungu hiki safari mbili au tatu, ili kila mtu apate kufikiria kuhusu ni kitu gani Biblia inachosema.

"Kwa sababu neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi, bali kwetu sisi tunaokolewa na nguvu ya Mungu kwa maana imeandikwa:

Nitaiharibu hekima yao wenye hekima na akili zao wenye akili nitazikataa."

"Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mleta hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu? Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuuzi wa lile Neno lililohubiriwa ……. Bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe

wenye heshima, tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyevye nguvu."

Jinsi tunavyo yaangalia maisha ya Kristo, tunaweza kuona kwamba njia za Mungu sio njia za mwanadamu.

- Wakati mfalme wa kidunia anapozaliwa, huwa anazaliwa katika jumba la kifalme. Kwa hali yoyote, Mungu alimtuma Yesu, mfalme wa wafalme, kuzaliwa katika umaskini.

- Wakati mtu fulani atatangaza ujumbe ulio muhimu ama kuwasili kwa mtu mashuhuri, mhudumu huyu ni tajiri, amevaa vizuri na anaendeshwa kuzungushwa katika gari muhimu. Mungu alimtuma Yohana Mbatizaji akivaa singa za ngamia kuja kutangaza kuwasili kwa Yesu katika jangwa mahali watu ilibidi watoke na kwenda njia ndefu ili kusikia matangazo yake.

- Wakati mfalme wa kibinadamu anapokuwa na adui ambaye anaweza akamshinda kirahisi, huwa anammaliza mara moja. Yesu bila haraka alikwenda jangwani ili akajaribiwe na Shetani. Na bado hakumharibu Shetani.

- Wakati mfalme wa kibinadamu anapochagua msaidizi wake wa karibu, huchagua watu ambao wamehitimu kutoka shule zilizo bora, wanaotoka familia bora na wale walio na mapesa mengi. Yesu alichagua, miongoni mwa kazi zingine za kawaida, wavuvi na watoza ushuru.

- Mfalme wa kiulimwengu huwalazimisha watu wake wamtii na huwaadhibu wale waliomsaliti. Yesu alitufundisha sisi upendo. Yesu anawaruhusu watu kuchagua kumfuata yeye au kumkataa.

- Mfalme wa kibinadamu huwafanya wengine wamfanyie kazi, walipe kodi na baadhi hata huwaua wale ambao ni wahaini kwa serikari yake. Yesu alikufa msalabani kwa makusudi kwa sababu alitaka kulipa gharama kwa ajili ya dhambi zetu. Yesu anataka sisi tuwe huru na tuishi milele pamoja na yeye.

- Wakati mfalme wa kidunia anapofariki, huwa anazikwa na mwanae huchukua mahali plae. Wakati Yesu alipofariki, alifufuka tena na anatawala milele.

  Yesu sio binadamu. Yeye ni Mungu. Yeye anapaswa kuabudiwa, kusujudiwa na kumtii. Yesu anatupenda sisi na anatutakia mema sisi. Maisha yake hapa duniani ni kwa ujumla hayana kifani. Njia za Mungu ni kubwa mno kuliko akili ndogo zinazoweza kufahamu na kwamba ziko butu kwa watu.

- Biblia inatufundisha kwamba mojawapo ya mambo ambayo Bwana anayoyapenda ni kusikia sifa za watu wake. Kusifu kwa kawaida na maana ya kumwambia Yesu ni kiasi gani wewe unampenda Yesu na unafurahia mambo yote ya kustaajabisha ambayo ndivyo ilivyo. Mungu

anapenda kusikia vitu kama, “Mimi nakupenda kwa sababu wewe ulinipenda au mimi ninakutukuza wewe Bwana ni mkuu na mwenye uwezo.” Hizi ni dondoo ambazo zinamwambia Mungu yeye ni nani kwangu binafsi.

Jinsi tunavyofikiria kuhusu maisha na kifo cha Kristo, sisi tunaweza tukafurahia kwa kufikiria ni kitu gani Mungu, muumba wa ulimwengu alifanya kwa ajili yetu. Njia zake ni kubwa mno na bora kuliko kitu chochote ambacho sisi hatuwezi hata kukitambua. Huu ndio wakati mwafaka kusimama kwa muda na kumtukuza Mungu. Kusudi la kusulubiwa kwake ilikuwa ni sadaka kwa ajili ya dhambi zetu. Yesu aliadhibiwa, akahukumiwa na kufa kwa ajili ya dhambi ambayo wewe umetenda na utatenda. Sisi lazima tumshukuru na tumtukuze Yesu kila siku kwa kuwa Bwana na Mwokozi.

Tutakwenda kufanya kitu kinaitwa “Maombi ya sentensi” maombi ya sentensi ni wakati kila mmoja anaomba kwa sentensi kwa wakati mmoja jinsi mawazo yanavyomjia katika akili kwamba angependa kujieleza kwa Mungu. Ebu sote tuinamishe vichwa vyetu na kufikiria kuhusu Mungu. Ni kipi Yesu alichokifanya wakati wa huduma yake duniani. Ni kipi Yesu alichokifanya juu ya msalaba, juu ya kurudi kwake, na anafanya nini sasa hivi katika maisha yetu. Kisha na tuchukue zamu, kuweka katika maneno mawazo yetu kuelekea Mungu. Kwa mfano, “Kisha mtu mwingine anasema sentensi

nyingine, “Baba mpendwa, wewe ni Baba mwenye huruma kwangu.” Kila mtu anaweza na anapashwa kuomba mara nyingi jinsi anavyojisikia akiongozwa na Roho. Huu ndio wakati wa kushiriki hadharani yale yaliyo moyoni mwentu. Endelea kama muda utakavyohitajika. Kisha hamia kwenye mahitaji ya maombi na omba kwa ajili ya mtu mwingine.

- *Kiongozi – wakumbushe wajumbe kuanza kujumlisha muda wa kumtukuza kila siku katika muda wao wa upweke na Mungu. Hakikisha unawaulizawajumbe kila juma jinsi gani muda wao wa upweke unavyoendelea. Watie moyo wale ambao wanayo shida na uwaruhusu watu kuchangia mambo ambayo Mungu amewaonyesha au vitu nadhifu ambavyo Mungu amewafanyia.*

UFUFUO WA KRISTO

MATHAYO

SOMO LA 8

"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zetu za mwisho." Yeremia 29:11

MARUDIO

1. Nabii Isaya alisema kwamba Yesu angeitwa Imanueli ikiwa na maana ya Mungu _____ _____.

2. Yesu alisema kwamba hakuna ajuaye ni lini yeye atarudi ulimwenguni ila ni _____.

3. Yohana aliwabatiza wengi huko jangwani ambao walitubu juu ya _____ zao.

4. Yesu alimjibu Shetani safari tatu akitumia _____ la _____.

5. ikiwa sisi tunataka kukua na kuwa karibu na Mungu na tuweze kupinga majaribu lazima sisi tutumie muda wa _____ pamoja na yeye _____.

6. Yesu aliwaita wafuasi wake kuwa wavuvi wa _____.

7. Yesu aliwaambi wafuasi wake kwenda nje katika jina lake wakiwa na busara kama _____ wawe wasio na madhara kama _____.

8. Petro alimsaliti Yesu kwa _____ yeye safari tatu katika ua ya Kayafa.

9. Yuda alimsaliti Yesu kwa kumtoa kwa makuhani kwa vipande _____.

10. Yesu _____ dhambi zetu zote wakati sisi tunapomkiri Yesu.

11. Askari wa Kirumi walimtendeaje Yesu?

12. Wakuu wa Makuhani walikuja paliposimikwa msalaba _____ Yesu anavyo aga dunia.

13. Kulikuwako na matukio mengi ya ajabu wakati Yesu alipofariki ikiwemo watu wengi waliokufa ambao _____ kuzunguka mji wa Yerusalemu.

14. Yusufu wa Arimathaya aliutwaa mwili wa Yesu kuulaza katika _____.

Siku iliyofuata baada ya Yesu kusulubiwa, wakuu wa makuhani na mafarisayo wakamkusanya Pilato. Wakamwambia Pilato kwamba Yesu alitabiri kwamba angefufuka kutoka katika wafu siku ya tatu. Wakamuomba ikiwa ulinzi mkali ungaliwekwa

kuhakikisha kwamba hakuna yeyote anauiba huo mwili. Pilato akakubali maombi yao, hivyo kundi la watu wakaenda kwenye kaburi na kuweka mhuri kwenye jiwe kubwa ambalo lilikingwa kwenye lango la kuingilia ndani ya pango. Pia waliwaacha hapo walinzi wenye silaha pale kuchunga mahali pale.

Sasa, siku baada ya Sabato, ambayo ni siku ya kwanza ya juma, Maria Magdalena na Maria yule mwingine walikwenda kulitazama kaburi. Wakati walipofika pale kulikuwa na tetemeko kubwa la nchi, na lile jiwe ambalo lilikuwa linakinga mlango wa kuingia ndani ya kaburi limeondolewa. Malaika wa Bwana ambaye ameshuka chini kutoka mbinguni alikuwa amekaa juu ya jiwe lile, lililotumika kuweka mhuri kaburini.

Nguo za malaika zilikuwa nyeupe kama theluji, na malaika alionekana kama kwamba alikuwa ni umeme. Wale maaskari ambao wamekuwa wakilinda kaburi walikuwa vilevile wapo pale wakitetemeka kwa woga mpaka wakawa kama wafu.

Malaika akawaambia wale wanawake wasiogope. Akasema, “Kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulubiwa. Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyo sema. Njoni mpatazame mahali Bwana alipolazwa. Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, amefufuka katika wafu. Tazama, awatangulia kwenda Galilaya, ndiko mtakakomwona huko. Haya, nimekwisha waambia.”

Wale wanawake, kwa kusikia haya wakajawa na furaha wakaenda mbio kurudi kwa wanafunzi. Walipokuwa njiani Yesu akakutana nao akisema, “Furahini!” Hivyo wakasimama wakakaribia kumshika miguuni na wakamsujudia yeye. Yesu aliwakumbusha wale wanawake kuwaambia wanafunzi kukutana na Yesu huko Galilaya.

Wakati huo, walinzi wakasimama na wakaenda zao mjini kuwaambia makuhani wakuu kila kitu ambacho kimetokea. Wakuu wa makuhani wakakusanyika pamoja ili kuwapa walinzi fedha nyingi kwa wao kuzunguka-zunguka na kusambaza neno kwamba wao walilala usingizi na ya kwamba watu wameiiba maiti ya Yesu.

Makuhani ndipo walipoahidi kuwalinda walinzi hao ikiwa Pilato atagundua na wakiwa katika matata. Hivyo ma-askari wakazitwaa zile fedha na uvumi huo ukaenea kuzunguka Yerusalemu kwa miaka mingi.

Wale wanafunzi wakaenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu kwenda Yesu akaja kwao, nao wakamsujudia. Lakini baadhi wakaona shaka. Ndipo Yesu akasema nao maagizo yake ya mwisho kabla ya kupaa kwake mbinguni. Yesu alisema, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, la Mwanza na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.” Amen.

MASWALI YA MDOMO

1. Ni kwa nini Mafarisayo walitaka kuweka walinzi kwenye kaburi la Yesu?

2. Ni wanawake gani wawili waliokuja kwenye eneo la kaburi?

3. Hawa wanawake waliona nini wakati walipofika pale kaburini?

4. Malaika aliwaambia nini wale wanawake?

5. Kulitokea nini kwa walinzi?

6. Walinzi walikwenda wapi baada ya malaika kutokea?

7. Walinzi walipewa tuzo gani na wakuu wa makuhani?

8. Wanawake walimwona nani wakati walipokuwa wanakimbia kurudi kwenda kukutana na wanafunzi?

9. Ni mahali gani Yesu alipowaambia wanafunzi wake kukutana naye?

10. Ilikuwa ni amri gani ambayo Yesu alitoa kwa wanafunzi wake juu ya mlima kabla hajapaa?

11. Ni nani Yesu aliyeahidi kuwa naye tangia saa mpaka mwisho wa dahari?

KWELI ZA KIROHO
MATHAYO 28

SOMO LA 8

1. **Ujumbe wa Yesu ni wakushirikisha kwa watu wote.** Inawezekana kwamba Mungu amekuwa akifanya kazi katika moyo wako akikupatia nguvu na shauku ya kushirikisha ujumbe wake na wengine. Zipo njia nyingi za kuwaambia wengine kuhusu upendo wa kristo. Njia moja nzuri ni kuongoza mtu au kundi la watu, kupitia hadithi ya maisha ya Yesu. Wewe unaweza kutumia masomo ya majuma saba ya "Habari Njema ya Yesu" kukusaidia wewe kushirikisha imani yako. Tangu fundisho

la nne tumekuwa kama kikundi, tukiomba kwa ajili ya watu dhahiri ambao Mungu amewaweka juu ya moyo wako. Kwa matumaini makubwa wewe umepata nafasi ya kuwaambia watu hawa machache kuhusu mabadiliko ambayo yametokwa katika maisha yako. Ikiwa sivyo, fanya hili liwe ni juma la kuwaendea.

- Usimwendee mtu huyu na kumwambia kwa kiasi gani wao ni watu wa ajabu na kwamba Mungu anakwenda kuwatuma moto usiozimika iwapo hawatatubu. Wewe lazima umwendee rafiki yako katika njia nzuri.

- Uwaalike wao kufanya masomo ya Biblia mafupi pamoja na wewe katika makao yao. Waambie kwamba umekuwa ukijifunza kuhusu Biblia na ulikuwa unajiuliza ikiwa huenda wangefurahi katika kujifunza pamoja na wewe maisha ya Kristo kwa majuma saba.

- Wakati unapokwenda kwa makao yao, uende na mshiriki pamoja nawe. Huenda akawa mtu fulani kutoka kwa kikundi chako cha Masomo ya Biblia au mtu ambaye mmekutana naye kanisani. Kiongozi wako wa masomo ya Biblia huenda akapenda kufuatana nawe.

- Wakati unapokwenda, tumia muda kwa kuzungumzia kwa mtu yule kuhusu mambo yanavyoenenda katika maisha yao. Kutana na familia, sikiliza mahitaji yao. Omba kwa ajili yao, kazi zao, familia zao na muombe Mungu kuleta amani yake juu ya mji wao.

- Anza na hadithi ya kwanza inayohusu kuzaliwa kwa Yesu. Waruhusu wao

kuuliza maswali. Ikiwa wewe haujui jibu hakuna shida. Wewe waambie kuwa utauliza kiongozi wako wa Masomo ya Biblia kwa sababu wewe haujui na kisha lete juma lijalo.

- Usikae kwa mji wao kwa zaidi ya saa moja. Kumbuka haya ni Masomo ya Biblia mafupi.

- Kila siku juma lile na kila juma baadaye, omba kwa ajili ya mtu huu na familia yake. Waombe wajumbe wa kikundi chako kujiunga nawe katika maombi kwa ajili yao.

KUMBUKA: Jinsi kama sisi tusivyo na uwezo wa kuponya au kutoa pepo yoyote, sisi hatuna uwezo wowote wa kushawishi watu kwa hitaji lao la Kristo. Yule mmoja aliye na uwezo ni Roho Mtakatifu anayeishi ndani yetu sisi. Yeye anao uwezo wa kuponya watu maradhi yao, yeye anao uwezo wa kutoa pepo kutoka kwa maisha ya watu na yeye ndiye ambaye anavunja minyororo ya dhambi katika maisha ya mtu na huwaleta watu kutubu katika Kristo. Jukumu letu sisi ni kushirikisha na kuomba.

Inawezekana kwamba wewe uko katika hali ambayo hauna nafasi ya kufanya Masomo ya Biblia ya majuma saba pamoja na mtu lakini

ungependa kushirikisha pamoja na wengine kuhusu Yesu Kristo.

JAMBO LA KUFANYA:

- Waeleze kwa uzuri jinsi uwezavyo kukumbuka, hadithi ya Kristo. Waeleze kuhusu kuzaliwa kwake, ubatizo wake, maisha yake, miujiza yake, upendo wake ujumbe wake wa toba, kusalitiwa kwake, kifo chake na ufufuo wake. Hii ina umuhimu wa peke yake ikiwa mtu huyu hana uzoefu wowote wa Kikiristo huko nyuma.

- Waeleze kwamba kama watu katika nyakati za Yesu, sisi sote tumefanya vibaya mbele za Mungu, hata ikiwa sisi ni watu wema. Hii ina maana kwamba sote tumetenda dhambi. Wape mifano ya baadhi ya dhambi: Kusema uongo, kuiba, chuki, husuda, uzinzi n.k.

- Waeleze kwamba kama vile Mungu alivyo wasamehe watu katika Biblia, yeye alikusamehe wewe wakati ulipotubu dhambi zako.

- Eleza machache kuhusu maisha yako kabla ya Kristo, wakti ulipochagua kumfuata Kristo na maisha ya tangu Kristo alipotawala maisha yako (Ushuhuda wako.)

- Simulia au soma moja ya mistari muhimu sana katika Biblia, Yohana 3:16 inasema, “Kwa maana jinsi hii, Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”

- Muulize yule mtu ikiwa wao pia wangependa kutubu juu ya dhambi zao, kuamini katika Kristo na kupokea msamaha ambao Yesu anaweza kuwapa.

- Eleza kwamba kuamini inamaana ya kugeuza maisha yako kwa Kristo. Hii ni kutegemea na kuweka maisha yako mikononi mwa Yesu.

- Ikiwa watasema, “Hapana” waulize ikiwa wangekuruhusu wewe kuomba kwa ajili yao kwa wakati huo, kisha omba kwa Mungu kwamba atawadia kuelewa ukweli wake kwa ajili ya maisha yao.

- Simama na ujipe muda wakati kundi linafanya zoezi ya kufikisha Yesu kwa mtu mwingine. Wagawanye katika vikundi vya wawili na acha kila mtu apitie mawasilisho yote.

Baada ya kufanya mazoezi, wewe unaweza ukafikiria, “Hii haiwezekani, mimi siwezi kamwe kumwambia yeyote kuhusu Kristo.” Fikiria kuhusu huu ukweli wa mwisho katika somo hili.

2. **Na lazima, mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dhahiri:** Biblia inatufundisha kwamba, tunapompokea Kristo, Roho Mtakatifu wa Mungu anakuja na kukaa ndani ya maisha yetu. Wewe unaweza ukawa haujatambua hii, lakini yeye tayari yuko kazini maisha yako (yohana 14:17).

    - Yeye ndiye yule aliyetufundisha katika muda wetu wa upweke pamoja na Mungu kila siku (Yohana 14:26).

    - Yeye ndiye yule ambaye anatufanya tujisikie kuwa na hatia wakati tunapokataa kumtii Mungu. Yeye ndiye yule aliyetuwezesha sisi kuelewa kwa mara ya kwanza kwamba sisi tu watenda dhambi na tulihitaji msamaha wa kristo katika maisha yetu (Yohana 16:8-11)

    - Yeye ndiye yule anayetupatia hekima na anatuongoza sisi katika mapenzi sahihi ya Mungu (Yohana 16:13).

    - Yeye ndiye yule anayetufariji wakati tunapokuwa na huzuni (Matendo 9:31)

- Yeye ndiye yule atutiaye nguvu pamoja na vipawa maalumu ili tuweze kufanya mambo ambayo kamwe hata tusingeliota kufanya. Yeye hutupatia maneno ya kuwaambia wengine kuhusu kristo (1Wakorintho 12).

Sisi tunaweza kufikiria kwamba kamwe hatuwezi kuwa aina ya wafuasi wa Kristo ambao tunahitaji tuwe. Sisi tunaweza kufikiria kwamba kumtii Mungu ni jambo lisilowezekana. Ukweli ni kwamba hii ni kweli. Sisi wenyewe hatuwezi kufanya chochote kumfuata kristo, **lakini Mungu anaweza** kupitia kwa Roho Mtakatifu anaishi katika maisha yetu.

Hii ndiyo siri ya kuwaambia kuhusu kristo, ndiyo siri ya kuishi maisha pasipo woga, ndio siri kwa kufanya maamuzi yalito sahihi kila siku. Wakati tulipomruhusu Muumba wa ulimwengu kuingia ndani ya maisha yetu, yeye alitupatia sisi kipawa, uwepo wake daima. Uwepo wa Roho Mtakatifu ndicho chanzo chetu cha nguvu na uwezo. Hii ni jambo la kufurahisha kwa sababu Biblia inatufundisha sisi kwamba Mungu anayo mipango ya kutisha, ana mawazo yasiyo sadikika na kusudi zuri kwa kila moja ya maisha yetu. Ebu tukamilishe somo hili kwa ahadi maalum inayopatikana katika Yeremia 29:11-13

"Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, Asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho. Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba nami nitawasikiliza. Nanyi mtanifuata na kuniona mtakaponifuata kwa moyo wenu wote."

MUNGU AKUBARIKI JINSI UNAVYOZIDI KUENDELEA KUMTAFUTA NA KUMJUA YEYE.

<u>UKWELI WA INJILI HAUBADILIKI LAKINI MITAZAMO HUBADILIKA KULINGANA NA UTAMADUNI</u>

KUMBUKA: Katika jamii ya kikristo unaweza kuendelea kutumia maswali ya milele. Lakini katika jamii ya wasio amini utatakiwa kutumia utambuzi katika kutambua kiwango cha uelewa wa kiroho. Uelewa wa mtu katika neno kama vile mbinguni linaweza kuwa ni tofauti na lile la kwenye Biblia.

Kuiwakilisha Injili

(Mistari sita inayoeleza ukuu wa injili.)

1. Kusudi la Mungu katika maisha yako

Biblia inasema katika I Yohana **5:13, "Nimewaandikia ninyi mambo hayo ili mjue ya kuwa mnao uzima wa milele ninyi mlioliamini jina la Mwana wa Mungu."**

Kusudi la mstari: Mungu anataka kutupa hakika ya maisha ya milele kwa sababu ya upendo wake kwa mwanadamu.

Maelezo ya mstari: Maisha ya milele ni vitu viwili:

a) Kumjua Yesu na kuwa na amani yake ktika moyo wako wakati ukiwa katika maisha haya. (Yohana 17:3)
b) Kuishi na Yesu Kristo mbinguni milele baada ya kufa (Yohana 14:1-3)

Matumizi ya Mstari: Unatakiwa kujua kwa uhakika kwamba unao uzima wa milele ?

Angalizo: Kwa Wakristo na wasio Wakristo maelezo haya yanatakiwa kuwa wazi kimaelezo na inaweza kukuchukua muda.

2. Hitaji lako

Biblia inasema katika **Warumi 3:23**, **"Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu".**

Kusudi la mstari huu: Ni kuonesha kwamba wote wana dhambi.

Maelezo ya mstari: Dhambi ni nini? Dhambi ni kutomtii Mungu. Kwa mfano, wote sisi tumefanya dhambi kama vile uongo, hasira, urafi, majivuno n.k.

Matumizi ya mstari huu: Unatambua ya kwamba umefanya dhambi na ni nini madhara ya dhambi?

Biblia inasema katika warumi **6:23, "Mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu."**

Kusudi la mstari: Unaonesha kwamba wote tunastahili mauti kwa sababu tumetenda dhambi.
Maelezo ya Mstari: mauti ni nini? Ina maana ya kutengana na Mungu katika njia mbili.

> Kwanza, mauti ni kutengana na Mungu sasa katika maisha ya duniani hapa. Ni maisha yasiyo na furaha au amani katika Roho. Ni maisha yasiyo na uhakika wa uzima wa milele na bila Yesu katika roho yako. Utengano wa Mungu humwacha mwanadamu akiwa tupu na roho yenye woga.
>
> Pili, mauti ni utengano na Mungu milele katika jehanamu. Haya ni maisha bila Yesu milele yote.

Kulingana na Biblia sisi sote tunastahili mauti, na kutengana na Mungu kwa sababu ya dhambi zetu.

Matumizi ya Mstari: Unaelewa kwamba unastahili kufa kwa sababu ya dhambi zako?

3. Pendo la Mungu

Biblia inasema katika Warumi **5:8, "Bali Mungu aonesha pendo lake kwetu sisi wakati tungali wenye dhambi, Kristo akafa kwa ajiri yetu."**

Kusudi a mstari: kuonesha kwamba Mungu anatupenda sana hata akamtoa mwana wake Yesu Kristo akafa kwa ajiri ya dhambi zetu.

Maelezo ya mstari: Mshahara wa dhambi ni mauti. Yesu Kristo aliadhibiwa akahukumiwa na kuuawa msalabani ili alipe gharama ya dhambi zetu.
Kifo cha Yesu kilikuwa ni dhabihu kamili ili kumweka huru mwanadamu kutoka katika dhambi. Watu wengi wanajaribu kumfikia Mungu kwa njia nyingi: wakitegema kazi zao, maisha yao mazuri, Wanajaribui kumfikia Mungu kwa njia ya utakatifu, sanamu, michoro, roho chafu na wafu. Juhudi za mwanadamu hazina nguvu za kutakasa dhambi yake. Njia ya kuweka ushirika na Mungu ni kupitia Yesu tu. Baada ya Yesu kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, alifufuka kutoka wafu akayashinda mauti. Yu hai na anataka aingie na kuishi katika maisha yako.

Matumizi ya Mstari huu: Unaamini kwamba Yesu ni Bwana wako, Mwokozi na mpatanishi?

4. Jukumu lako

Biblia inasema katika Warumi **10: 9, "Kwamba ukimkiri Yesu kwa kinywa chako na kuamini moyoni mwako ya kwamba Yesu ni Bwana na kwamba Mungu alimfufua katika wafu utaokoka."**

Kusudi la mstari: Ni kukuonesha cha kufanya ili upate kumpokea Yesu kama Bwana wako
Maelezo ya mstari: Kumpokea Yesu unatakiwa kufanya mambo mawili:

a) Kwanza, Kumpokea Yesu unapaswa kukiri kwamba yeye ni Bwana wako tu. Uzikatae dhambi zako na ugeuke kumfuata Yesu. Hii inamaana kuacha kuendesha maisha yako na kumpa Yesu. Na hii ni toba

b) Pili, kumpokea Yesu unapaswa kuamini moyoni mwako kwamba Yesu alifufuka katika wafu na kwamba yeye ni mwokozi wako. Ina maana kwamba unapaswa kuacha kuamini mambo mengine kama vile kazi nzuri,vinyago, sanamu, utakatifu au wafu na uweke imani yako kwa Yesu kama Mwokozi wako .

Matumizi ya Mstari: Uko tayari kumkiri Yesu kama Bwana na mwokozi wako na umkabidhi maisha yako kama Bwana? Je uko tayari kuacha kuabudu vitu vingine na umpe Kristo maisha yako sasa kama Bwana na Mwokozi wako?

Biblia inasema katika Warumi **10:13, "Atakayeliitia jina la Bwana ataokoka."**

Kusudi la mstari: Ni kuonesha kwamba yeyote atakayeliitia jina la Bwana ataokoka.

Maelezo ya Mstari: Unaweza kumpokea Yesu sasa kwa imani katika moyo wako.

Matumizi ya mstari: Uko tayari kumkabidhi Yesu na umwombe aingie katika maisha yako sasa? Kama uko tayari sema sala hii kwa moyo wako mbele za Mungu.

> "Bwana, Mimi ni mwenye dhambi, ninakuamini Bwana, kama Bwana wangu tu, mwokozi na mpatanishi, ninayatoa maisha yangu kwako. Ingia katika moyo wangu na uniokoe sasa, nigeuze na uyaongoze maisha yangu yote. Amen."

Unaamini kwamba Yesu amejibu maombi yako? Umeokoka?